# NOTISI YA TARATIBU ZA ULINZI WA HAKI

**(2016)**

## KWA WANAFUNZI WALIO NA ULEMAVU NA WAZAZI WAO

## KWA MUJIBU WA SHERIA YA WATU WALIO NA ULEMAVU

# NOTISI YA TARATIBU ZA ULINZI WA HAKI

Mpendwa Mzazi,

Waraka huu unakupa notisi inayohitajika ya taratibu za ulinzi zilizopo kwa mujibu wa Individuals with Disabilities Education Act (Sheria ya Elimu ya Watu walio na Ulemavu, IDEA) na kanuni za Idara ya Elimu ya marekani. IDEA, sheria ya Serikali Kuu kuhusu elimu ya wanafunzi walio na ulemavu, inahitaji shule kumpa mzazi wa mtoto aliye na ulemavu notisi iliyo na ufafanuzi kamili wa taratibu za ulinzi zilizopo. Lazima nakala ya notisi hii itolewe mara moja tu kwa kila mwaka wa shule, isipokuwa lazima pia nakala itolewe:

(a) Kwa rufaa ya mwanzo au ombi lako la tathmini;
(b) Kwa kupokea malalamishi yako ya kwanza ya Jimbo na kwa kupokea malalamishi yako ya kwanza ya utaratibu wa kina katika mwaka wa shule;
(c) Wakati uamuzi umetolewa ili kuchukua hatua ya nidhamu dhidi ya mtoto wako inayohitaji mabadiliko ya alikowekwa; na
(d) Kwa ombi lako.

**Tafadhali wasiliana na wilaya ya shule kwa maelezo zaidi kuhusu haki hizi:**

*Weka lebo hapa*

**Kwa ufafanuzi zaidi unaweza kuwasiliana na:**
**Idaho Special Education Dispute Resolution, State Dept. of Education**
P.O. Box 83720 Boise, ID 83720-0027
Simu: (208) 332-6914
Faksi: (208) 334-2228
Wavuti: www.sde.idaho.gov Simu ya bila malipo: (800) 432-4601
V/TT: (800) 377-3529

**Kwa usaidizi wa masuala yanayohusiana na suluhisho la mgogoro, unaweza kuwasiliana na:**

***DisAbility Rights Idaho Boise Office***
9542 W. Bethel Court
Boise, ID 83709-0569
Simu: (208) 336-5353
Simu ya bila malipo: (800) 632-5125
Faksi: (208) 336-5396
Wavuti: disabilityrightsidaho.org

***Idaho Legal Aid Services***
1447 Tyrell Lane
Boise, ID 83706
Simu: (208) 336-8980
Faksi: (208) 342-2561
Wavuti: idaholegalaid.org

***DisAbility Rights Idaho Pocatello Office***
1246 Yellowstone Ave Suite A-3
Pocatello, ID 83201-4374
Simu: (208) 232-0922
Simu ya bila malipo: (866) 309-1589
Faksi: (208) 232-0938
Wavuti: disabilityrightsidaho.org

***Idaho State Bar Association***
P.O. Box 895 Boise, ID 83701
Simu (208) 334-4500
Faksi: (208) 334-4515
Wavuti: isb.idaho.gov

***Idaho Parents Unlimited, Inc. (IPUL)***
4619 Emerald, Ste. E Boise, ID 83702
Simu: (208) 342-5884
Simu ya bila malipo: (800) 242-IPUL (4785)
V/TT: (208) 342-5884
Faksi: (208) 342-1408
Wavuti: ipulidaho.org

***Wrightslaw Idaho Yellow Pages for Kids***
Wavuti: yellowpagesforkids.com/help/id.htm

# ***TAARIFA ZA JUMLA***

***NOTISI ILIYOANDIKWA MAPEMA***
***34 CFR §300.503***
**Notisi**
Lazima wilaya ya shule yako ikupe notisi iliyoandikwa (ikupe taarifa fulani kwa maandishi), ndani ya muda unaofaa kabla ya:

1. Kupendekeza kuanzisha au kubadilisha utambulisho, tathmini au mazingira ya elimu ya mtoto wako, au utoaji wa elimu ya umma inayofaa bila malipo (FAPE) kwa mtoto wako; **au**
2. Kukataa kuanzisha au kubadilisha utambulisho, tathmini au mazingira ya elimu ya mtoto wako, au utoaji wa FAPE kwa mtoto wako.

**Maudhui ya notisi**
Lazima notisi iliyoandikwa:

3. Ieleze hatua ambayo wilaya ya shule yako inapendekeza au inakataa kuchukua;
4. Ieleze sababu ya wilaya yako ya shule kupendekeza au kukataa kuchukua hatua;
5. Ieleze kila utaratibu wa tathmini, uchunguzi, rekodi au ripoti ambayo wilaya ya shule yako ilitumia kuamua kupendekeza au kukata hatua;
6. Ijumuishe kauli kwamba una ulinzi kwa mujibu wa vipengele vya utaratibu wa ulinzi katika Sehemu ya B ya IDEA;
7. Ikuambie jinsi unavyoweza kupata maelezo ya taratibu za ulinzi ikiwa hatua ambayo wilaya ya shule yako inapendekeza au inakataa si rufaa ya mwanzo kwa ajili ya tathmini;
8. Ijumuishe huduma za wewe kuwasiliana nazo kwa usaidizi wa kuelewa Sehemu ya B ya IDEA;
9. Ieleze chaguo jingine lolote ambalo timu ya mtoto wako ya mpango wa elimu iliyobinafsishwa (IEP) ilizingatia na sababu za machaguo hayo kukataliwa; **na**
10. Itoe maelezo ya sababu nyingine za wilaya ya shule yako kupendekeza au kukataa hatua.

**Notisi kwa lugha inayoeleweka**
Lazima notisi:

1. Iandikwe kwa kugha inayoeleweka kwa umma kwa jumla;
   **na**
2. Itolewe kwa lugha yako asili au njia nyingine ya mawasiliano unayotumia, isipokuwa isiwezekane kabisa kufanya hivyo.

Ikiwa lugha yako ya asili au njia nyingine ya mawasiliano si lugha ya maandishi, lazima wilaya ya shule yako ihakikishe kwamba:

1. Notisi imetafsiriwa kwa ajili yako kwa njia ya mdomo au kwa njia nyingine katika lugha yako ya asili au mbinu nyingine ya mawasiliano;
2. Unaelewa maudhui ya notisi; na
3. Kuna ushahidi wa maandishi wa kuonyesha kwamba matakwa yaliyo kwenye aya ya 1 na 2 yametimizwa.

***LUGHA ASILI***
***34 CFR §300.29***
*Lugha asili*, inapotumiwa kuhusu mtu ambaye ana ustadi mdogo wa Kiingereza, inamaanisha yafuatayo:

1. Kwa kawaida lugha hutumiwa na mtu huyo, au ikiwa ni mtoto, kwa kawaida lugha hutumiwa na wazazi wa mtoto;
2. Katika mawasiliano yote ya moja kwa moja na mtoto (ikiwa ni pamoja na tathmini ya mtoto), kwa kawaida lugha hutumiwa na mtoto nyumbani au shuleni.

Kwa mtu aliye na matatizo ya kusikia au kuona, au kwa mtu asiye na lugha ya maandishi, njia ya mawasiliano ni ile ambayo kwa kawaida mtu huyo hutumia (kama vile lugha ya ishara, Breli, au mawaisliano ya mdomo).

***BARUA PEPE***
***34 CFR §300.505***
Ikiwa wilaya ya shule yako inawapa wazazi chaguo la kupokea nyaraka kwa njia ya barua pepe, unaweza kuchagua kupokea zifuatazo kwa njia ya barua pepe:

1. Notisi iliyoandikwa mapema;
2. Notisi ya taratibu za ulinzi; **na**
3. Notisi zinazohusiana na malalamishi ya mchakato wa haki.

***IDHINI YA MZAZI - UFAFANUZI***
***34 CFR §300.9***
**Idhini**
*Idhini* inamaanisha:
1. Umefahamishwa kikamilifu kwa lugha yako asili au njia nyingine ya mawasiliano (kama vile lugha ya ishara, Breli, au mawasiliano ya mdomo) kuhusu taarifa zote kuhusu hatua ambayo unatolea idhini.
2. Unaelewa na unakubali hatua hiyo kwa njia ya maandishi na kwamba idhini inaeleza hatua hiyo na kuorodhesha rekodi (ikiwa zipo) zitakazotolewa na zinazotolewa kwake; **na**
3. Unaelewa kuwa idhini ni ya hiari kwako na kwamba unaweza kuiondoa wakati wowote.

Ikiwa ungependa kubatilisha (kughairi) idhini yako baada ya mtoto wako kuanza kupokea elimu maalum na huduma husika, lazima ufanye hivyo kwa njia ya maandishi. Uamuzi wako wa kuiondoa idhini haukanushi (hautangui) hatua ambayo imetokea baada ya kutoa idhini yako ila kabla ya kuiondoa. Vilevile, wilaya ya shule haihitajiki kurekebisha (kubadilisha) rekodi za elimu ya mtoto wako ili kuondoa marejeo yoyote kwamba mtoto wako alipokea elimu maalum na huduma husika baada ya uamuzi wako wa kuiondoa idhini yako.

***IDHINI YA MZAZI***
***34 CFR §300.300***
**Idhini ya tathmini ya mwanzo**
Wilaya ya shule yako haiwezi kufanya tathmini ya mwanzo ya mtoto wako ili kuamua ikiwa mtoto wako anastahiki kwa mujibu wa Sehemu ya B ya IDEA kupokea elimu maalum na huduma husika bila kwanza kukupa notisi ya maandishi ya hatua inayopendekezwa na kupata idhini yako kama ilivyoelezwa chini ya vichwa ***Notisi ya Maandishi ya Mapema*** na ***Idhini ya Mzazi.***

Lazima wilaya ya shule yako ifanye jitihada zinazofaa ili kupata idhini yako ya ufahamu kwa ajili ya tathmini ya mwanzo kuamua ikiwa mtoto wako ni mtoto mwenye ulemavu.

Idhini yako kwa tathmini ya mwanzo haimaanishi kwamba pia umetoa idhini yako kwa wilaya ya shule kuanza kumpa mtoto wako elimu maalum na huduma husika.

Wilaya ya shule yako haitatumia hatua yako ya kukataa kutoa idhini ya huduma au shughuli moja inayohusiana na tathmini ya mwanzo kama msingi wa kukunyima wewe au mtoto wako huduma, fidia, au shughuli nyingine yoyote, isipokuwa matakwa mengine ya Sehemu ya B yahitaji wilaya ya shule kufanya hivyo.

Ikiwa mtoto wako amesajiliwa katika shule ya umma au unataka kumsajili mtoto wako katika shule ya umma na umekataa kutoa idhini au umeshindwa kujibu ombi la kutoa idhini kwa ajili ya tathmini ya mwanzo, wilaya ya shule yako inaweza kuomba kufanya tathmini ya mwanzo ya mtoto wako, lakini haihitajiki, kwa kutumia upatanishi au malalamishi ya mchakato wa haki, mkutano wa suluhisho na taratibu za usikilizaji wa kesi ya mchakato wa haki bila upendeleo. Wilaya ya shule yako haitakiuka majukumu yake ya kutafuta, kutambua na kumtathmini mtoto wako ikiwa haitafanya tathmini ya mtoto wako katika hali hizi.

**Sheria maalum za tathmini ya mwanzo ya mtoto aliye chini ya ulinzi wa Jimbo**

Ikiwa mtoto yuko chini ya ulinzi wa Jimbo na haishi na mzazi wake —

Wilaya ya shule haihitaji idhini kutoka kwa mzazi kwa ajili ya tathmini ya mwanzo ya kuamua ikiwa mtoto ni mtoto mwenye ulemavu ikiwa:

1. Licha ya jitihada zinazofaa za kufanya hivyo, wilaya shule haiwezi kumpata mzazi wa mtoto;
2. Haki za wazazi zimesimamishwa kwa mujibu wa sheria ya Jimbo; au
3. Jaji amehawilisha haki ili kufanya maamuzi ya elimu hadi kwa mtu ambaye si mzazi na mtu huyo ametoa idhini ya tathmini ya mwanzo.

***Mtoto chini ya ulinzi wa Jimbo***, kama inavyotumiwa katika IDEA, inamanisha mtoto ambaye, kama ilivyoamuliwa na Jimbo mahali mtoto anapoishi:

1. Ni mtoto wa kulea;
2. Anachukuliwa kuwa mtoto aliye chini ya ulinzi wa Jimbo kwa mujibu wa sheria ya Jimbo; **au**
3. Katika ulinzi wa shirika la maslahi ya watoto la umma.

Kuna kighairi kimoja unachopaswa kujua. Mtu aliye chini ya ulinzi wa Jimbo hajumuishi mtoto wa kulea ambaye ana mzazi mlezi anayekidhi ufafanuzi wa mzazi kama unavyotumika katika IDEA.

**Idhini ya mzazi kwa ajili ya huduma**

Lazima wilaya yako ya shule ipate idhini yako ya ufahamu kabla ya kumpa mtoto wako elimu maalum na huduma husika kwa mara ya kwanza.

Lazima wilaya ya shule ifanye jitihada zinazofaa ipate idhini yako ya ufahamu kabla ya kumpa mtoto wako elimu maalum na huduma husika kwa mara ya kwanza.

Usipojibu ombi la kutoa idhini yako ili mtoto wako apokee elimu maalum na huduma husika kwa mara ya kwanza, au ukikataa kutoa idhini hiyo au ubatilishe (ughairi) baadaye idhini yako kwa njia ya maandishi, wilaya ya shule yako haitatumia taratibu za ulinzi (yaani, upatanishi, malalamishi ya mchakato wa haki, mkutano wa suluhisho, au usikilizaji kesi ya mchakato wa haki bila upendeleo) ili kupata makubaliano au uamuzi unaosema kuwa mtoto wako anaweza kupata elimu maalum na huduma husika (zilizopendekezwa na Timu ya IEP ya mtoto wako) bila idhini yako. Ukikataa kutoa idhini yako ili mtoto wako apokee elimu maalum na huduma husika kwa mara ya kwanza, au usipojibu ombi la kutoa idhini hiyo au ubatilishe (ughairi) baadaye idhini yako kwa njia ya maandishi na wilaya ya shule isimpe mtoto wako elimu maalum na huduma husika ambazo inahitaji idhini yako, wilaya ya shule yako:

1. Haikiuki matakwa ya kumpa mtoto wako elimu ya umma inayofaa bila malipo (FAPE) kwa kushindwa kwake kumpa mtoto wako huduma hizo; **na**
2. Haihitajiki kufanya mkutano wa mpango wa elimu iliyobinafsishwa (IEP) wala kuunda IEP kwa ajili ya mtoto wako ya elimu maalum na huduma husika zilizokuwa zikihitaji ombi lako.

Ukibatilisha (ukighairi) idhini yako kwa njia ya maandishi wakati wowote baada ya mtoto wako kupewa elimu maalum na huduma husika, basi wilaya ya shule haitaendelea kutoa huduma hizo, lakini lazima ikupe notisi iliyoandikwa mapema, kama ilivyoelezwa chini ya kichwa ***Notisi Iliyoandikwa Mapema***, kabla ya kusimamisha huduma hizo.

**Haki za Mzazi Kupinga**

Mara baada ya kuidhinisha kuanza kwa huduma, wilaya ya shule haihitajiki kupata idhini yako ili kufanya mabadiliko kwenye IEP. Hata hivyo, ikiwa hutaki wilaya ya shule kutekeleza mabadiliko kwenye IEP, lazima uwasilishe pingamizi zako kwa njia ya maandishi. Lazima pingamizi zako kwa njia ya maandishi ziwe na muhuri wa posta au ziwasilishwe kwa mkono kwenye wilaya ya shule ndani ya siku 10 za kupokea notisi iliyoandikwa kuhusu mabadiliko.

IDAPA 8.02.03.109.0Sa

**Idhini ya mzazi kwa ajili ya tathmini mpya**

Lazima wilaya ya shule yako ipate idhini yako ya ufahamu kabla haijamtathmini upya mtoto wako, isipokuwa wilaya ya shule yako iweze kuonyesha kwamba:

1. Ilichukua hatua zinazofaa kupata idhini yako kwa ajili ya tathmini mpya ya mtoto wako; **na**
2. Hukujibu.

Ukikataa kuidhinisha tathmini mpya ya mtoto wako, wilaya ya shule inaweza kufanya tathmini mpya ya mtoto wako, ila haihitajiki kufanya hivyo, kwa kutumia upatanishi, malalamishi ya mchakato wa haki, mkutano wa suluhisho na taratibu za kesi ya mchakato wa haki bila upendeleo ili kuomba kupuuza hatua yako ya kukataa kuidhinisha tathmini mpya ya mtoto

wako. Kama ilivyo kwenye tathmini za mwanzo, wilaya ya shule yako haikiuki majukumu yake kwa mujibu wa Sehemu ya B ya IDEA ikikataa kufanya tathmini mpya kwa njia hii.

**Nyaraka za jitihada zinazofaa za kupata idhini ya mzazi**

Lazima shule yako ihifadhi nyaraka za jitihada zinazofaa za kupata idhini yako kwa ajili ya tathmini za mwanzo, ili kutoa elimu maalum na huduma husika kwa mara ya kwanza, kwa tathmini mpya na kuwapata wazazi wa watoto walio chini ya ulinzi wa Jimbo kwa tathmini za mwanzo. Lazima nyaraka zijumuishe rekodi ya majaribio ya wilaya ya shule katika sehemu hizi, kama vile:

1. Rekodi za maelezo ya kina ya simu zilizopigwa au zilizojaribiwa na matokeo ya simu hizo;
2. Nakala za barua uliyotumiwa na majibu yoyote yaliyopokelewa; **na**
3. Rekodi za maelezo ya kina kuhusu ziara zilizofanywa nyumbani au kazini kwako na matokeo ya ziara hizo.

**Matakwa mengine ya idhini**

Idhini yako haihitajiki kabla ya wilaya ya shule yako:

1. Kukagua data iliyopo ya tathmini au tathmini mpya ya mtoto wako; **au**
2. Kumpa mtoto wako mtihani au tathmini nyingine inayopewa watoto wengine wote isipokuwa, kabla ya mtihani au tathmini hiyo, idhini inahitajika kutoka kwa wazazi wa watoto wote.

Lazima wilaya ya shule iunde na kutekeleza taratibu za kuhakikisha kwamba hatua yako ya kukataa kuidhinisha huduma na shughuli yoyote kati ya hizi haisababishi kushindwa kumpa mtoto wako elimu ya umma inayofaa bila malipo (FAPE). Pia, wilaya ya shule yako haitatumia hatua yako ya kukataa kutoa idhini ya huduma au shughuli moja kama msingi wa kunyima huduma, fidia, au shughuli nyingine yoyote, isipokuwa matakwa mengine ya Sehemu ya B yahitaji wilaya ya shule kufanya hivyo.

Ikiwa umemsajili mtoto wako kwenye shule ya binafsi kwa gharama yako mwenyewe au ukiwa unamfundishia mtoto wako nyumbani na ukose kutoa idhini ya tathmini ya mwanzo au tathmini mpya ya mtoto wako, au ushindwe kujibu ombi la kutoa idhini yako, wilaya ya shule haitatumia taratibu zake za suluhisho la mgogoro (yaani, upatanishi, maalamishi ya mchakato wa haki, mkutano wa suluhisho, au kesi ya mchakato wa haki bila upendeleo) na haihitajiki ya kumchukulia mtoto wako kwamba anastahiki kupokea huduma sawa (huduma zinazoweza kupatikana kwa watoto wengine wenye ulemavu wa shule ya binafsi waliowekwa na wazazi wao binafsi.

***TATHMINI HURU ZA ELIMU***

***34 CFR §300.502***

**Jumla**

Kama ilivyoelezwa hapa chini, una haki ya kupata tathmini huru ya elimu (IEE) ya mtoto wako ikiwa unapinga tathmini ya mtoto wako iliyofanywa na wilaya ya shule yako. Ukiomba tathmini huru ya elimu, lazima wilaya ya shule ikupe taarifa kuhusu mahali unapoweza kupata tathmini huru ya elimu na kuhusu vigezo vya wilaya ya shule vinavyotumika kwenye tathmini huru za elimu.

**Fafanuzi**

Tathmini huru ya elimu inamaanisha tathmini iliyofanywa na mtahini aliyehitimu ambaye hajaajiriwa na wilaya ya shule inayoshughulikia elimu ya mtoto wako.

Gharama ya umma inamaanisha kwamba wilaya ya shule inalipia gharama yote ya tathmini au inahakikisha kwamba unapewa tathmini bila malipo, kwa mujibu wa vipengele vya Sehemu ya B ya IDEA, ambavyo vinaruhusu kila Jimbo kutumia vyanzo vyovyote vya msaada wa Jimbo, serikali za mitaa, Serikali Kuu na vya binafsi vilivyopo katika Jimbo ili kukidhi matakwa ya Sehemu ya B ya Sheria.

**Haki ya tathmini kwa gharama ya umma**

Una haki ya tathmini huru ya elimu ya mtoto wako kwa gharama ya umma ikiwa unapinga tathmini iliyofanywa na wilaya ya shule yako, kwa kuzingatia masharti yafuatayo:

1. Ukiomba tathmini huru ya elimu ya mtoto wako kwa gharama ya umma, lazima wilaya ya shule yako, bila kuchelewa kusikohitajika: (a) Iwasilishe malalamishi ya mchakato wa haki kuomba usikilizaji kesi ili kuonyesha kwamba tathmini yake ya mtoto wako inafaa; **au** (b) Itoe tathmini huru ya elimu kwa gharama ya umma, isipokuwa wilaya ya shule ionyeshe katika kesi kuwa tathmini ya mtoto wako iliyofanywa haikukidhi vigezo vya wilaya ya shule.
2. Ikiwa wilaya ya shule yako inaomba usikilizaji kesi na uamuzi wa mwisho unasema kuwa tathmini ya wilaya ya shule

yako ya mtoto wako inafaa, bado una haki ya kupata tathmini huru ya elimu, lakini si kwa gharama ya umma.

3. Ukiomba tathmini huru ya elimu ya mtoto wako, wilaya ya shule inaweza kukuomba sababu ya kupinga tathmini ya mtoto wako iliyofanywa na wilaya ya shule yako.

4. Hata hivyo, huenda wilaya ya shule yako isihitaji ufafanuzi na haiwezi kuchelewesha kumfanyia mtoto wako tathmini huru ya elimu bila sababu kwa gharama ya umma au kuwasilisha malalamishi ya mchakato wa haki ili kuomba usikilizaji kesi ya mchakato wa haki ili kutetea tathmini ya wilaya ya shule ya mtoto wako.

Una haki ya tathmini huru ya elimu moja tu ya mtoto wako kwa gharama ya umma kila wakati wilaya ya shule yako inapofanya tathmini ya mtoto wako ambayo unapinga.

**Tathmini zilizoanzishwa na mzazi**

Ukipata tathmini huru ya elimu ya mtoto wako kwa gharama ya umma au ukishiriki na wilaya ya shule tathmini ya mtoto wako ambayo ulipata kwa gharama ya binafsi:

1. Lazima wilaya ya shule yako izingatie matokeo ya tathmini ya mtoto wako, ikiwa yanakidhi vigezo vya wilaya ya shule vya tathmini huru za elimu, katika uamuzi wowote unaotolewa kulingana na kipengele cha elimu ya umma inayofaa bila malipo (FAPE) kwa mtoto wako; **na**
2. Wewe au wilaya ya shule yako inaweza kuwasilisha tathmini kama ushahidi kwenye kesi ya mchakato wa haki kumhusu mtoto wako.

**Maombi ya tathmini na mahakimu**

Ikiwa afisa wa usikilizaji kesi ataomba tathmini huru ya elimu ya mtoto wako kama sehemu ya usikilizaji kesi ya mchakato wa haki, lazima gharama ya tathmini iwe ya umma.

**Vigezo vya wilaya ya shule**

Ikiwa tathmini huru ya elimu ni kwa gharama ya umma, vigezo ambavyo tathmini imetumia, ikiwa ni pamoja na eneo la tathmini na sifa za mtahini, lazima viwe sawa na vigezo ambavyo wilaya ya shule hutumia inapoanzisha tathmini (kwa kiwango ambapo vigezo hivyo vinalingana na haki yako ya tathmini huru ya elimu).

Isipokuwa kwa vigezo vilivyoelezwa hapo juu, wilaya ya shule haitaweka masharti wala muda unaohusiana na kufanya tathmini huru ya elimu kwa gharama ya umma.

## ***USIRI WA TAARIFA***

***USIRI WA TAARIFA***
***34 CFR §300.502***
Kama ilivyotumika chini ya kichwa **Usiri wa Taarifa:** ***Uharibifu*** inamaanisha uhairbifu wa kitu halisi au uondoaji wa vitambulishi kwenye taarifa ili taarifa hizo zisitambulike binafsi.
***Rekodi za elimu*** inamaanisha aina ya rekodi zinazolindwa chini ya ufafanuzi wa ''rekodi za elimu'' katika 34 CFR Sehemu ya 99 (kanuni zinazotekeleza Sheria ya Haki na Faragha ya Elimu ya Familia ya 1974, 20 U.S.C. 1232g (FERPA)).
***Shirika linaloshiriki*** inamaanisha wilaya yoyote ya shule, shirika au taasisi inayokusanya, kuhifadhi au kutumia taarifa zinazotambulisha binafsi au ambako taarifa zimetolewa, kwa mujibu wa Sehemu ya B ya IDEA.

***ZINAZOTAMBULISHA BINAFSI***
***34 CFR §300.32***
Zinazotambulisha binafsi inamaanisha taarifa zinazojumuisha:
(a) Jina la mtoto wako, jina lako ukiwa mzazi, au jina la mwanafamilia mwingine;
(b) Anwani ya mtoto wako;
(c) Kitambulishi cha binafsi, kama vile nambari ya ruzuku ya serikali ya mtoto wako au nambari ya mwanafunzi; **au**
(d) Orodha ya sifa za binafsi au taarifa nyingine ambazo zitawezesha kumtambua mtoto wako kwa uhakika unaofaa.

***NOTISI KWA WAZAZI***
***34 CFR §300.612***
Lazima Shirika la Elimu la Jimbo litowe notisi ya muda unaofaa ili kuwafahamisha wazazi kikamilifu kuhusu usiri wa taarifa zinazotambulisha binafsi, ikiwa ni pamoja na:
1. Maelezo ya kiwango ambacho notisi inatolewa katika lugha asili za makundi ya watu mbalimbali katika Jimbo;
2. Maelezo ya watoto ambao taarifa za kutambulisha binafsi zinahifadhiwa, aina za taarifa zinazohitajika, mbinu ambazo Jimbo linakusudia kutumia kukusanya taarifa (ikiwa ni pamoja na vyanzo ambavyo taarifa zinakusanywa) na matumizi ya taarifa zenyewe;
3. Muhtasari wa sera na taratibu ambazo mashirika yanayoshiriki lazima yafuate kuhusu hifadhi, ufichuzi kwa wahusika wengine, uzuiaji na uharibifu wa taarifa zinazotambulisha binafsi; **na**
4. Maelezo ya haki zote za wazazi na watoto kuhusu taarifa hizi, ikiwa ni pamoja na haki kwa mujibu wa Sheria ya Haki na Faragha ya Elimu ya Familia (FERPA) na kanuni zake za utekelezaji katika 34 CFR Sehemu ya 99.

Kabla ya shughuli yoyote kubwa ya kutambua, kutafuta au kutathmini watoto wanaohitaji elimu maalum na huduma husika (pia inayojulikana kama "child find"), lazima notisi ichapishwe au itangazwe katika magazeti au vyombo vingine vya habari, au vyote viwili, kwa usambazaji wa kutosha ili kuwaarifu wazazi katika Jimbo zima kuhusu shughuli hizi.

***HAKI ZA UFIKIAJI***
***34 CFR §300.613***
Lazima shirika linaloshiriki likuruhusu kuchunguza na kukagua rekodi zozote za elimu zinazohusiana na mtoto wako ambazo zinakusanywa, kuhifadhiwa, au kutumiwa na wilaya ya shule kwa mujibu wa Sehemu ya B ya IDEA. Lazima shirika linaloshiriki litii ombi lako la kuchunguza na kukagua rekodi zozote za elimu kumhusu mtoto wako bila ucheleweshaji usiohitajika na kabla ya mkutano wowote kuhusu mpango wa elimu iliyobinafsishwa (IEP) au kesi yoyote ya mchakato wa haki bila upendeleo (ikiwa ni pamoja na mkutano wa suluhisho au kesi kuhusu nidhamu) na bila kupitisha siku 45 za kalenda baada yako kutuma ombi.
Haki yako ya kuchunguza na kukagua rekodi za elimu ni pamoja na:
1. Haki yako ya kupata jibu kutoka kwenye shirika linaloshiriki kwa maombi yako yanayofaa kwa ajili ya ufafanuzi na ufasiri wa rekodi zako;
2. Haki yako ya kuomba shirika linaloshiriki litoe nakala za rekodi ikiwa huwezi kuchunguza na kukagua kwa ufanisi rekodi isipokuwa upokee nakala hizo; **na**
3. Haki yako ya mwakilishi wako kuchunguza na kukagua rekodi.

Shirika linaloshiriki linaweza kuchukulia kwamba una mamlaka ya kuchunguza na kukagua rekodi zinazohusiana na mtoto wako isipokuwa lifahamishwe kwamba huna mamlaka kwa mujibu wa sheria ya Jimbo inayotumika ambayo inaongoza masuala kama ulezi, kutengana na talaka.

***REKODI YA UFIKIAJI***
***34 CFR §300.614***
Lazima kila shirika linaloshiriki lihifadhi rekodi za wahusika wanaofikia rekodi za elimu zilizokusanywa, kuhifadhiwa na kutumika kwa mujibu wa Sehemu ya B ya IDEA (isipikuwa ufikiaji wa wazazi na waajiriwa walioidhinishwa wa shirika linaloshiriki), ikiwa ni pamoja na jina la mhusika, tarehe ambayo idhini ya ufikiaji ilitolewa na madhumuni ya mhusika kuidhinishwa kutumia rekodi.

***REKODI KUHUSU ZAIDI YA MTOTO MMOJA***
***34 CFR §300.615***
Ikiwa rekodi yoyote ya elimu inajumuisha taarifa kuhusu zaidi ya mtoto mmoja, wazazi wa watoto hao wana haki ya kuchunguza na kukagua tu taarifa zinazohusiana na mtoto wao au kufahamishwa kuhusu taarifa hiyo mahususi.

***ORODHA YA AINA NA MAENEO YA TAARIFA***
***34 CFR §300.616***
Kwenye ombi, lazima kila shirika linaloshiriki likupe orodha ya aina na maeneo ya rekodi zilizokusanywa, kuhifadhiwa au kutumiwa na shirika.

***ADA***
***34 CFR §300.617***
Kila shirika linaloshiriki linaweza kutoza ada kwa nakala za rekodi ambazo unapewa kwa mujibu wa Sehemu ya B ya IDEA, ikiwa ada haikuzuii kutumia haki yako ya kuchunguza na kukagua rekodi hizo.
Shirika linaloshiriki halitatoza ada ya kutafuta au kurejesha taarifa kwa mujibu wa Sehemu ya B ya IDEA.

***MAREKEBISHO YA REKODI KWA OMBI LA MZAZI***
***34 CFR §300.618***
Ikiwa unaamini kwamba taarifa zilizo katika rekodi za elimu kuhusu mtoto wako zilizokusanywa, kuhifadhiwa na kutumiwa kwa mujibu wa Sehemu ya B ya IDEA si sahihi, zinapotosha au zinakiuka faragha au haki nyingine za mtoto wako, unaweza kuomba shirika linaloshiriki ambalo linahifadhi taarifa lizibadilishe taarifa.
Lazima shirika linaloshiriki liamue ikiwa litabadilisha taarifa kwa mujibu wa ombi lako ndani ya kipindi kinachofaa cha kupokea ombi lako.
Ikiwa shirika linaloshiriki litakataa kubadilisha taarifa kwa mujibu wa ombi lako, lazima likufahamishe kuhusu ukataaji na kukushauri kuhusu haki ya usikilizaji kesi kama ilivyoelezwa chini ya kichwa **Fursa ya Usikilizaji Kesi.**

***FURSA YA USIKILIZAJI KESI***
***34 CFR §300.619***
Lazima shirika linaloshiriki, likupe fursa ya usikilizaji kesi ili kupinga taarifa zilizo katika rekodi za elimu kumhusu mtoto wako kuhakikisha kwamba si sahihi, zinapotosha au zinakiuka faragha au haki nyingine za mtoto wako.

***TARATIBU ZA USIKILIZAJI KESI***
***34 CFR §300.621***
Usikilizaji kesi ya kupinga taarifa zilizo katika rekodi za elimu lazima ufanywe kwa mujibu wa taratibu za kesi hizi kulingana na Sheria ya Haki na Faragha ya Elimu ya Familia (FERPA).

***MATOKEO YA KESI***
***34 CFR §300.620***
Ikiwa, kutokana na kesi, shirika linaloshiriki litaamua kwamba taarifa si sahihi, zinapotosha au zinakiuka faragha au haki nyingine za mtoto wako, lazima lipinge taarifa ipasavyo na kukufahamisha kwa njia ya maandishi.

Ikiwa, kutokana na usikilizjai kesi, shirika linaloshiriki litaamua kwamba taarifa si sahihi, zinapotosha au zinakiuka faragha au haki nyingine za mtoto wako, lazima likufahamishe kuhusu haki yako ya kuweka katika rekodi ambazo linalohifadhi kumhusu mtoto wako ripoti inayotoa maoni kuhusu taarifa au kutoa sababu yoyote unayopinga uamuzi wa shirika linaloshiriki. Ufafanuzi kama huo uliowekwa katika rekodi za mtoto wako lazima:

1. Uhifadhiwe na shirika linaloshiriki kama sehemu ya rekodi za mtoto wako kwa muda ambao rekodi au sehemu

inayopingwa inahifadhiwa na shirika linaloshiriki; **na**

2. Ikiwa shirika linaloshiriki litafichua rekodi za mtoto wako au taarifa zinazopingwa kwa mhusika yeyote, lazima ufafanuzi pia ufichuliwe kwa mhusika huyo.

***IDHINI YA UFICHUZI WA TAARIFA ZINAZOTAMBULISHA BINAFSI***
***34 CFR §300.622***

Isipokuwa taarifa iwe katika rekodi za elimu na ufichuzi uidhinishwe bila idhini ya mzazi kulingana na Sheria ya Haki na Faragha ya Elimu ya Familia (FERPA), lazima idhini yako ichukuliwe kabla ya taarifa zinazotambulisha binafsi kufichuliwa kwa wahusika ambao si maafisa wa mashirika yanayoshiriki. Isipokuwa kulingana na hali zilizobainishwa hapa chini, idhini yako haihitajiki kabla ya taarifa zinazotambulisha binafsi kupewa maafisa wa mashirika yanayoshiriki kwa madhumuni ya kukidhi mahitaji ya Sehemu ya B ya IDEA.

Idhini yako, au idhini ya mtoto anayestahiki ambaye amefikisha umri unaokubalika kisheria kulingana na sheria ya Jimbo, lazima ipatikane kabla ya taarifa zinazotambulisha binafsi kupewa maafisa wa mashirika yanayoshiriki kutoa au kulipia huduma za mpito. Ikiwa mtoto wako yuko au ataenda kwenye shule ya binafsi ambayo haiko katika wilaya moja na shule unayokaa, lazima idhini yako ipatikane kabla ya taarifa yoyote inayotambulisha binafsi kumhusu mtoto wako kutolewa baina ya maafisa walio katika wilaya ya shule ambapo shule ya binafsi ipo na maafisa walio katika wilaya ya shule ambapo unakaa.

***ULINZI***
***34 CFR §300.623***

Lazima kila shirika linaloshiriki lilinde usiri wa taarifa zinazotambulisha binafsi kwenye hatua za ukusanyaji, hifadhi, ufichuaji na uharibifu.
Afisa mmoja katika kila shirika linaloshirki lazima awajibike kwa kuhakikisha usiri wa taarifa yoyote inayotambulisha binafsi.
Lazima watu wote wanaokusanya au wanaotumia taarifa zinazotambulisha binafsi wapokee mafunzo au maagizo kuhusu sera na taratibu za Jimbo lako kuhusu usiri kulingana na Sehemu ya B ya IDEA na Sheria ya Haki na Faragha ya Elimu ya Familia (FERPA).
Lazima kila shirika linaloshiriki lihifadhi, kwa ajili ya uchunguzi wa umma, orodha ya sasa ya majina na vyeo vya waajiriwa wote ndani ya shirika ambao wanaweza kufikia taarifa zinazotambulisha binafsi.

***UHARIBIFU WA TAARIFA***
***34 CFR §300.624***

Lazima wilaya ya shule yako ikufahamishe wakati taarifa zinazotambulisha binafsi zimekusanywa, zimehifadhiwa au kutumiwa kulingana na Sehemu ya B ya IDEA hazihitajiki tena ili kumpa mtoto wako huduma za elimu.
Lazima taarifa ziharibiwe kwa ombi lako. Hata hivyo, rekodi ya kudumu ya jina, anwani na nambari ya simu ya mtoto wako, gredi zake, rekodi ya mahudhurio, madarasa aliyohudhuria, kiwango cha gredi alichokamilisha na mwaka wa kukamilisha zinaweza kuhifadhiwa bila kikomo cha muda.

## ***TARATIBU ZA UTII WA JIMBO***

***TOFAUTI BAINA YA TARATIBU ZA MALALAMISHI YA MCHAKATO WA HAKI NA KESI NA MALALAMISHI YA JIMBO***

Kanuni za Sehemu ya B ya IDEA zilizobainishwa zinatenganisha taratibu za malalamishi ya Jimbo na za malalamishi ya mchakato wa haki na kesi. Kama ilivyofafanuliwa hapa chini, mtu au shirika lolote linaweza kuwasilisha malalamishi ya Jimbo likidai wilaya ya shule, Shirika la Elimu ya Jimbo, au shirika jingine lolote la umma kukiuka hitaji lolote la Sehemu ya B. Ni wewe au wilaya ya shule tu inayoweza kuwasilisha malalamishi ya mchakato wa haki kuhusu suala lolote linalohusiana na pendekezo au kukataa kuanzisha au kubadilisha utambulisho, tathmini au jaribio la elimu la mtoto aliye na ulemavu, au kipengele cha elimu ya umma inayofaa bila malipo (FAPE) kwa mtoto wako. Ingawa lazima wafanyakazi wa Shirika la Elimu la Jimbo wasuluhishe malalamishi ya Jimbo ndani ya kipindi cha siku 60 za kalenda, isipokuwa kipindi kirefushwe inavyofaa, lazima hakimu bila upendeleo asikilize malalamishi ya mchakato wa haki (ikiwa hayajasuluhishwa kupitia mkutano wa suluhisho au kupitia upatanishi) na kutoa uamuzi wa maandishi ndani ya siku 45 za kalenda baada ya

mwisho wa kipindi cha suluhisho, kama ilivyoelezwa katika waraka huu chini ya kichwa Mchakato wa Suluhisho, isipokuwa aruhusu urefushaji wa kipindi kwa ombi lako au ombi la wilaya ya shule. Taratibu za malalamishi ya Jimbo na malalamishi ya mchakato wa haki, taratibu za suluhisho na kesi zimeelezwa kikamilifu zaidi hapa chini. Lazima Shirika la Elimu ya Jimbo liunde fomu za modeli ili kukusaidia kuwasilisha malalamishi ya mchakato wa haki na kukusaidia au kuwasaidia wahusika wengine kuwasilisha malalamishi ya Jimbo kama ilivyoelezwa chini ya kichwa ***Fomu za Modeli***.

***KUKUBALI TARATIBU ZA MALALAMISHI YA JIMBO 34 CFR §300.151***

**Jumla**

Lazima kila Shirika la Elimu ya Jimbo liwe na taratibu zilizoandikwa za:

1. Kusuluhisha lalamishi lolote, ikiwemo lalamishi lililowasilishwa na shirika au mtu kutoka Jimbo jingine;
2. Kuwasilisha malalamishi kwenye Shirika la Elimu ya Jimbo;
3. Kusambaza kwa upana taratibu za malalamishi ya Jimbo kwa wazazi na watu wengine wanaohusika, ikiwemo vituo vya mafunzo na taarifa kwa wazazi, mashirika ya ulinzi na utetezi, vituo vya kujitegemea na taasisi nyingine zinazofaa.

**Suluhu za kunyimwa huduma zinazofaa**

Katika kusuluhisha malalamishi ya Jimbo ambapo Shirika la Elimu ya Jimbo limetambua kosa la kutotoa huduma zinazofaa, lazima Shirika la Elimu ya Jimbo lishughulikie:

1. Kosa la kutotoa huduma zinazofaa, ikiwa ni pamoja na hatua ya marekebisho inayofaa kushughulikia mahitaji ya mtoto (kama vile huduma za lazima au ufidiaji wa pesa); **na**
2. Utoaji wa huduma zinazofaa wa siku zijazo kwa watoto wote walio na ulemavu.

***TARATIBU ZA CHINI ZAIDI ZA MALALAMISHI YA JIMBO 34 CFR §300.152***

**Kikomo cha muda; taratibu za chini zaidi**

Lazima kila Shirika la Elimu ya Jimbo lijumuishe katika taratibu zake za malalamishi ya jimbo kikomo cha muda wa siku 60 za kalenda baada ya malalamishi kuwasilishwa ili:

1. Kufanya uchunguzi huru kwenye kituo, ikiwa Shirika la Elimu ya Jimbo litaamua kwamba uchunguzi unahitajika;
2. Kumpa mlalamishi fursa ya kuwasilisha taarifa zaidi, kwa njia ya mdomo au ya maandishi, kuhusu madai yaliyo katika malalamishi;
3. Kuipa wilaya ya shule au shirika jingine la umma fursa ya kujibu malalamishi, ikiwa ni pamoja na, kwa kiwango cha chini: (a) kwa chaguo la shirika, pendekezo la kusuluhisha malalamishi; **na** (b) fursa ya mzazi aliyewasilisha malalamishi na shirika kukubaliana kwa hiari kushiriki katika upatanishi;
4. Kukagua taarifa zote zinazofaa na kufanya uamuzi huru wa ikiwa wilaya ya shule au shirika jingine la umma linakiuka matakwa ya Sehemu ya B ya IDEA; **na**
5. Kumpa mlalamishi uamuzi ulioandikwa ambao unashughulikia kila dai lililo katika malalamishi na una: (a) uamuzi na maoni; **na** (b) sababu za uamuzi wa mwisho wa Shirika la Elimu ya Jimbo.

**Urefushaji wa muda; uamuzi wa mwisho; utekelezaji**

Taratibu za Shirika la Elimu ya Jimbo zilizoelezwa hapo juu pia lazima:

1. Ziruhusu urefushaji wa kikomo cha muda cha siku 60 za kalenda: (a) hali za kipekee zipo kuhusiana na malalamishi fulani ya Jimbo; **au** (b) wewe na wilaya ya shule au shirika jingine la umma lililohusika mlikubaliana kwa hiari kurefusha muda wa kusuluhisha suala kupitia upatanishi au njia mbadala ya suluhisho la mgogoro, ikiwa inapatikana katika Jimbo.
2. Jumuisha taratibu za utekelezaji bora wa uamuzi wa mwisho wa Shirika la Elimu ya Jimbo, ikihitajika, ikiwa ni pamoja na: (a) shughuli za usaidizi wa kiufundi; (b) majadiliano; **na** (c) hatua za urekebishaji ili kufanikisha utii.

***Malalamishi ya Jimbo na kesi za mchakato wa haki***

Ikiwa malalamishi yaliyoandikwa ya Jimbo yamepokelewa ambayo pia yanatokana na kesi ya mchakato wa haki kama ilivyoelezwa chini ya kichwa ***Kuwasilisha Malalamishi ya Mchakato wa Haki***, au malalamishi ya Jimbo yana masuala mengi ambapo moja au zaidi ni sehemu ya kesi hiyo, lazima Jimbo liweke kando sehemu yoyote ya malalamishi ya Jimbo ambayo yanashughulikiwa katika kesi ya mchakato wa haki hadi kesi iishe. Suala lolote katika malamishi ya Jimbo ambalo si sehemu ya kesi ya mchakato wa haki lazima lisuluhishwe kwa kutumia kikomo cha muda na taratibu zilizoelezwa hapo juu.

Ikiwa suala lililoibuliwa katika malalamishi ya Jimbo liliamuliwa awali katika kesi ya mchakato wa haki inayohusisha wahusika sawa (kwa mfano, wewe na wilaya ya shule), basi uamuzi wa kesi ya mchakato wa haki unabana kwenye suala hilo na lazima Shirika la Elimu ya Jimbo limfahamishe mlalamishi kuwa uamuzi unabana.
Malalamishi yanayodai kushindwa kwa wilaya ya shule au shirika jingine la umma kutekeleza uamuzi wa kesi ya mchakato wa haki lazima lisuluhishwe na Shirika la Elimu ya Jimbo.

***KUWASILISHA MALALAMISHI YA JIMBO***
***34 CFR §300.153***

Shirika au mtu anaweza kuwasilisha malalamishi yaliyoandikwa ya Jimbo kulingana na taratibu zilizoelezwa hapo juu.
Lazima malalamishi ya Jimbo yajumuishe:

1. Taarifa kuwa wilaya ya shule au shirika jingine la umma limekiuka matakwa ya Sehemu ya B ya IDEA au kanuni zake za kutekeleza katika 34 CFR Part 300;
2. Ukweli kwa msingi wa taarifa;
3. Sahihi na maelezo ya mawasiliano ya mhusika anayewasilisha malalamishi; na
4. Ikiwa anadai ukiukaji kuhusu mtoto mahususi:
   (a) Jina la mtoto na anwani ya makazi ya mtoto;
   (b) Jina la shule ambayo mtoto anasomea;
   (c) Ikiwa ni mtoto au kijana asiye na makao, maelezo ya mawasiliano ya mtoto yaliyopo na jina la shule ambayo mtoto anasomea;
   (d) Maelezo ya hali ya tatizo la mtoto, ikiwa ni pamoja na ukweli unaohusiana na tatizo; **na**
   (e) Suluhisho lililopendekezwa la tatizo kwa kiwango kinachojulikana na kinachopatikana kwa mhusika anayewasilisha malalamishi wakati malalamishi yanawasilishwa.

Lazima malalamishi yadai ukiukaji uliotokea si zaidi ya mwaka mmoja kabla ya tarehe ambayo malalamishi yamepokelewa kama ilivyoelezwa chini ya kichwa ***Kukubali Taratibu za Malalamishi ya Jimbo***. Mhusika anayewasilisha malalamishi ya Jimbo lazima atume nakala ya malalamishi kwenye wilaya ya shule au shirika jingine la umma linalomtumikia mtoto wakati mmoja mhusika anapowasilisha malalamishi kwenye Shirika la Elimu ya Jimbo.

## ***TARATIBU ZA MALALAMISHI YA MCHAKATO WA HAKI***

***KUWASILISHA MALALAMISHI YA MCHAKATO WA HAKI***
***34 CFR §300.507***

**Jumla**

Wewe au wilaya ya shule inaweza kuwasilisha malalamishi ya mchakato wa haki kuhusu suala lolote linalohusiana na pendekezo au kukataa kuanzisha au kubadilisha utambulisho, tathmini au jaribio la elimu la mtoto wako, au kipengele cha elimu ya umma inayofaa bila malipo (FAPE) kwa mtoto wako.
Lazima malalamishi ya mchakato wa haki yadai ukiukaji uliotendeka si zaidi ya miaka miwili kabla ya wewe au wilaya ya shule kujua au ilipaswa kujua kuhusu hatua inayodaiwa ambayo ndiyo msingi wa malalamishi ya mchakato wa haki.
Muda ulio hapo juu hautumiki kwako ikiwa hukuweza kuwasilisha malalamishi ya mchakato wa haki ndani ya muda kwa sababu:

1. Wilaya ya shule ilipotosha kwamba ilikuwa imesuluhisha masuala yalitotambuliwa katika malalamishi; au
2. Wilaya ya shule ilizuia taarifa kutoka kwako ambazo ihitajika kukupa chini ya Sehemu ya B ya IDEA.

**Taarifa za wazazi**

Lazima wilaya ya shule ikufahamisha kuhusu huduma yoyote inayofaa ya bila malipo au ya gharama ya chini na nyingine muhimu zinazopatikana katika eneo ukiomba taarifa, **au** ikiwa wewe au wilaya ya shule yako itawasilisha malalamishi ya mchakato wa haki.

***MALALAMISHI YA MCHAKATO WA HAKI***
***34 CFR §300.508***

**Jumla**

Ili kuomba usikilizaji wa kesi, wewe au wilaya ya shule (au wakili wako au wakili wa wilaya ya shule) lazima iwasilishe malalamishi ya mchakato wa haki kwa mhusika mwingine. Lazima malalamishi yawe na maudhui yote yaliyoorodheshwa

na yawekwe siri.
Yeyote anayewasilisha malalamishi lazima pia alipe Shirika la Elimu ya Jimbo nakala ya malalamishi.

**Maudhui ya malalamishi**
Lazima malalamishi ya mchakato wa haki yajumuishe:
1. Jina la mtoto;
2. Anwani ya makazi ya mtoto;
3. Jina la shule ya mtoto;
4. Ikiwa mtoto au kijana hana makao, maelezo ya mawasiliano ya mtoto na jina la shule ya mtoto;
5. Maelezo ya hali ya tatizo la mtoto linalohusiana na hatua inayopendekezwa au inayokataliwa, ikiwa ni pamoja na ukweli unaohusiana na tatizo; **na**
6. Suluhisho lililopendekezwa la tatizo kwa kiwango kinachojulikana na kinachopatikana kwa mhusika (wewe au wilaya ya shule) anayelalamika wakati huo.

**Notisi inahitajika kabla ya kesi kuhusu malalamishi ya mchakato wa haki**
Wewe au wilaya ya shule huenda isiwe na kesi ya mchakato wa haki hadi wewe au wilaya ya shule (au wakili wako au wakili wa wilaya ya shule) iwasilishe malalamishi ya mchakato wa haki ya taarifa zilizoorodheshwa hapo juu.

**Utoshelevu wa malalamishi**
Ili malalamishi ya mchakato wa haki yaendelee, lazima yasemekane kuwa toshelevu. Malalamishi ya mchakato wa haki yatasemekana kuwa toshelevu (kuwa yamekidhi matakwa ya maudhui yaliyo hapo juu) isipokuwa mhusika anayepokea malalamishi ya mchakato wa haki (wewe au wilaya ya shule) aarifu hakimu na mhusika mwingine kwa njia ya maandishi, ndani ya siku 15 za kalenda za kupokea malalamishi, kwamba mhusika anayepokea anaamini kwamba malalamishi ya mchakato wa haki hayakidhi matakwa yaliyoorodheshwa hapo juu.
Ndani ya siku tano za kalenda za kupokea arifa kuwa mhusika anayepokea (wewe au wilaya ya shule) anachukulia malalamishi ya mchakato wa haki kuwa si toshelevu, lazima hakimu aamue ikiwa malalamishi ya mchakato wa haki yanakidhi matakwa yaliyoorodheshwa hapo juu na kukuarifu wewe na wilaya ya shule kwa njia ya maandishi mara moja.

**Marekebisho ya malalamishi**
Wewe au wilaya ya shule inaweza kufanya mabadiliko kwenye malalamishi ikiwa tu:
1. Mhusika mwingine anaidhinisha mabadiliko kwa njia ya maandishi na anapewa nafasi ya kusuluhisha malalamishi ya mchakato wa haki kupitia mkutano wa suluhisho, ulioelezwa chini ya kichwa ***Mchakato wa Suluhisho***; **au**
2. Kufikia muda usiozidi siku tano kabla ya kesi ya mchakato wa haki kuanza, hakimu anatoa ruhusa ya mabadiliko.

Ikiwa mhusika anayelalamika (wewe au wilaya ya shule) atafanya mabadiliko kwenye malalamishi ya mchakato wa haki, muda wa mkutano wa suluhisho (ndani ya siku 15 za kalenda za kupokea malalamishi) na kipindi cha suluhisho (ndani ya siku 30 za kalenda za kupokea malalamishi) zinaanza tena tarehe ambayo malalamishi yaliyorekebishwa yanawasilishwa.

**Jibu la shirika la elimu ya serikali za mitaa (LEA) au wilaya ya shule kwa malalamishi ya mchakato wa haki**
Ikiwa wilaya ya shule haijakutumia notisi iliyoandikwa mapema, kama ilivyoelezwa chini ya kichwa ***Notisi Iliyoandikwa Mapema***, kuhusu suala lililo katika malalamishi yako ya mchakato wa haki, lazima wilaya ya shule ikutumie jibu ndani ya siku 10 za kalenda za kupokea malalamishi ya mchakato wa haki linalojumuisha:
1. Ufafanuzi wa sababu ya wilaya ya shule kupendekeza au kukataa kuchukua hatua iliyoibuliwa katika malalamishi ya mchakato wa haki;
2. Maelezo ya machaguo mengine ambayo Timu ya mtoto wako ya mpango wa elimu iliyobinafsishwa (IEP) ilizingatia na sababu za machaguo hayo kukataliwa;
3. Maelezo ya kila utaratibu wa tathmini, uchunguzi, rekodi au ripoti ambayo wilaya ya shule ilitumia kama msingi wa hatua iliyopendekezwa au iliyokataliwa; na
4. Maelezo ya mambo mengine ambayo ni muhimu kwa hatua iliyopendekezwa au iliyokataliwa na wilaya ya shule.

Kutoa taarifa katika vipengee 1-4 vilivyo hapo juu hakuzuii wilaya ya shule kusema kwamba malalamishi yako ya mchakato wa haki hayakuwa toshelevu.

**Jibu la mhusika mwingine kwa malalamishi ya mchakato wa haki**
Isipokuwa kama ilivyobainishwa chini ya kichwa kidogo kilicho hapo juu, **Jibu la shirika la elimu ya serikali za mitaa**

**(LEA) au wilaya ya shule kwa malalamishi ya mchakato wa haki**, mhusika anayepokea malalamishi ya mchakato wa haki lazima amtumie mhusika mwingine jibu ambalo linaangazia haswa masuala yaliyo katika malalamishi ndani ya siku 10 za kalenda za kupokea malalamishi.

***FOMU ZA MODELI***
***34 CFR §300.509***
Lazima Shirika la Elimu ya Jimbo liunde fomu za modeli ili kukusaidia kuwasilisha malalamishi ya mchakato wa haki na kukusaidia na kuwasaidia wahusika wengine kuwasilisha malalamishi ya Jimbo. Hata hivyo, huenda Jimbo au wilaya ya shule yako isihitaji kutumia fomu hizi za modeli. Unaweza kutumia fomu ya modeli au fomu nyingine inayofaa mradi tu iwe na taarifa zinazohitajika za kuwasilisha malalamishi ya mchakato wa haki au malalamishi ya Jimbo.

UPATANISHI
***34 CFR §300.506***
**Jumla**
Lazima wilaya ya shule iunde taratibu zinazowezeshe uwepo wa upatanishi ili kukuruhusu wewe na wilaya ya shule kusuluhisha tofauti zinazohusu jambo lolote kulingana na Sehemu ya B ya IDEA, ikiwa ni pamoja na mambo yanayoibuka kabla ya kuwasilisha malalamishi ya mchakato wa haki. Kwa hivyo, upatanishi unapatikana ili kusuluhisha migogoro kulingana na Sehemu ya B ya IDEA, iwe umewasilisha au hujawasilisha malalamishi ya mchakato wa haki kuomba kesi ya mchakato wa haki kama ilivyoelezwa chini ya ***Kuwasilisha Malalamishi ya Mchakato wa Haki.***

**Matakwa**
Lazima taratibu zihakikishe kwamba mchakato wa upatanishi:
(1) Ni wa hiari upande wako na upande wa wilaya ya shule;
(2) Haitumiki kunyima au kuchelewesha haki yako ya kesi ya mchakato wa haki, wala kukunyima haki nyingine yoyote iliyotolewa kulingana na Sehemu ya B ya IDEA; na
(3) Unafanywa na mpatanishi aliyehitimu na asiyependelea aliyepata mafunzo ya mbinu faafu za upatanishi.

Wilaya ya shule inaweza kuunda taratibu zinazowapa wazazi na shule zinazochagua kutotumia mchakato wa upatanishi, fursa ya kukutana, wakati na eneo linalokufaa, na mhusika asipendelea:

1. Ambaye ana mkataba na taasisi mbadala inayofaa ya suluhisho la migogoro, au kituo cha mafunzo na taarifa cha wazazi au kituo cha huduma za wazazi cha jamii katika Jimbo; na
2. Ambaye atakufafanulia faida za na kuhimiza matumizi ya mchakato wa upatanishi.

Lazima Jimbo lihifadhi orodha ya watu ambao ni wapatanishi waliohitimu na kujua sheria na kanuni zinazohusiana na utoaji wa elimu maalum na huduma husika. Lazima Shirika la Elimu ya Jimbo lichague wapatanishi kwa msingi wa kubahatisha, kubadilisha au mwingine usiopendelea.
Jimbo linalipia gharama za mchakato wa upatanishi, ikiwa ni pamoja na gharama za mikutano.
Lazima kila mkutano katika mchakato wa upatanishi uratibiwe wakati unaofaa na kufanyika katika eneo ambalo linakufaa wewe na wilaya ya shule.
Ikiwa wewe na wilaya ya shule mtasuluhisha mgogoro kupitia mchakato wa upatanishi, lazima wahusika wote wawili wawe kwenye makubaliano yanayobana kisheria ambayo yanabainisha suluhisho na:

1. Yanabainisha kwamba majadiliano yote yaliyofanyika wakati wa mchakato wa upatanishi yatasalia ya siri na hayatatumiwa kama ushahidi katika kesi yoyote ya mchakato wa haki unaofuata au kesi ya raia (kesi ya mahakama); na
2. Yanatiwa sahihi na wewe na mwakilishi wa wilaya ya shule aliye na mamlaka ya kubana wilaya ya shule.

Makubaliano ya upatanishi yaliyoandikwa na kutiwa sahihi yanaweza kutekelezwa katika mahakama yoyote ya Jimbo yenye uwezo (mahakama yaliyo na mamlaka kulingana na sheria ya Jimbo kusikiliza aina hii ya kesi) au katika mahakama ya wilaya ya Marekani.
Majadiliano yaliyofanyika wakati wa mchakato wa upatanishi lazima yawe ya siri. Hayawezi kutumiwa kama ushahidi katika kesi yoyote ya mchakato wa haki ya siku zijazo wala kesi ya raia ya mahakama yoyote ya Serikali kuu au ya Jimbo ya Jimbo linalopokea usaidizi kulingana na Sehemu ya B ya IDEA.

**Uadilifu wa mpatanishi**
Mpatanishi:
1. Hapaswi kuwa mwajiriwa wa Shirika la Elimu ya Jimbo wala wilaya ya shule ambayo inahusika katika elimu au utunzaji wa mtoto wako; na
2. Hapaswi kuwa na maslahi ya binafsi au ya taaluma ambayo yanagongana na lengo la mpatanishi.

Mtu ambaye anahitimu kuwa mpatanishi si mwajiriwa wa wilaya ya shule wala shirika la Jimbo kwa sababu analipwa na shirika au wilaya ya shule ili ahudumu kama mpatanishi.

***MCHAKATO WA SULUHISHO***
***34 CFR §300.510***
**Mkutano wa suluhisho**
Ndani ya siku 15 za kalenda za kupokea notisi ya malalamishi yako ya mchakato wa haki na kabla ya kesi ya mchakato wa haki kuanza, lazima wilaya ya shule iandae mkutano nawe na mshirika au washirika husika wa Timu ya mpango wa elimu iliyobinafsishwa (IEP) walio na maarifa mahususi ya mambo halisi yaliyotambuliwa katika malalamishi yako ya mchakato wa haki. Mkutano:
1. Lazima ujumuishe mwakilishi wa wilaya ya shule aliye na mamlaka ya kufanya uamuzi kwa niaba ya wilaya ya shule; **na**
2. Haupaswi kujumuisha wakili wa wilaya ya shule isipokuwa uwe umeandamana na wakili.

Wewe na wilaya ya shule mnaamua washirika husika wa Timu ya IEP wa kuhudhuria mkutano.
Madhumuni ya mkutano ni kwa ajili yako kujadili malalamishi yako ya mchakato wa haki na mambo halisi ambayo ndiyo msingi wa malalamishi, ili wilaya ya shule ipate fursa ya kusuluhisha mgogoro.
Mkutano wa suluhisho si lazima ikiwa:
1. Wewe na wilaya ya shule mnakubaliana kwa njia ya maandishi kuondoa mkutano; **au**
2. Wewe na wilaya ya shule mnakubaliana kutumia mchakato wa upatanishi, kama ilivyoelezwa chini ya kichwa ***Upatanishi***.

**Kipindi cha suluhisho**
Ikiwa wilaya ya shule haijasuluhisha malalamishi ya mchakato wa haki kwa kiwango kinachokuridhisha ndani ya siku 30 za kalenda za kupokea malalamishi ya mchakato wa haki (kipindi cha mchakato wa suluhisho), kesi ya mchakato wa haki inaweza kutokea.
Muda wa siku 45 za kalenda za kutoa uamuzi wa kesi ya mchakato wa haki, kama ilivyolezwa chini ya kichwa, Maamuzi ya Kesi, unaanza mwisho wa kipindi cha suluhisho cha siku 30 za kalenda, bila kuhusisha mambo mengine kwa marekebisho yaliyofanywa kwenye kipindi cha suluhisho la siku 30 za kalenda, kama ilivyoelezwa hapa chini.
Isipokuwa pale ambapo wewe na wilaya ya shule mmekubaliana kuondoa mchakato wa suluhisho au kutumia upatanishi, kukosa kwako kushiriki katika mkutano wa suluhisho kutacheleweshа muda wa mchakato wa suluhisho na kesi ya mchakato wa haki hadi mkutano ufanyike.
Ikiwa baada ya kufanya jitihada zinazofaa na kurekodi jitihada hizo, wilaya ya shule imeshindwa kupata idhini ya ushiriki wako katika mkutano wa suluhisho, huenda wilaya ya shule ikaomba hakimu atupilie mbali malalamishi yako ya mchakato wa haki mwishoni mwa kipindi cha suluhisho cha siku 30 za kalenda. Lazima rekodi ya jitihada kama hizo ijumuishe rekodi ya majaribio ya wilaya ya shule kupanga wakati na mahali mlipokubaliana kama vile:
1. Rekodi za maelezo ya kina ya simu zilizopigwa au zilizojaribiwa na matokeo ya simu hizo;
2. Nakala za barua uliyotumiwa na majibu yoyote yaliyopokelewa; na
3. Rekodi za maelezo ya kina kuhusu ziara zilizofanywa nyumbani au kazini kwako na matokeo ya ziara hizo.

Ikiwa wilaya ya shule itashindwa kuandaa mkutano wa suluhisho ndani ya siku 15 za kalenda za kupokea notisi ya malalamishi yako ya mchakato wa haki **au** ikishindwa kushiriki katika mkutano wa suluhisho, unaweza kuomba hakimu kuanza muda wa kesi ya mchakato wa haki wa siku 45 za kalenda.

**Marekebisho kwenye kipindi cha suluhisho cha siku 30 za kalenda**
Ikiwa wewe na wilaya ya shule mnakubaliana kwa njia ya maandishi kuondoa mkutano wa suluhisho, basi muda wa siku 45 za kalenda kwa ajili ya kesi ya mchakato wa haki utaanza siku inayofuata.
Baada ya kuanza kwa upatanishi au mkutano wa suluhisho na kabla ya mwisho wa kipindi cha suluhisho cha siku 30 za kalenda, ikiwa wewe na wilaya ya shule mnakubaliana kwa njia ya maandishi kwamba hakuna makubaliano

yanayowezekana, basi muda wa siku 45 za kalenda kwa ajili ya kesi ya mchakato wa haki unaanza siku inayofuata.
Ikiwa wewe na wilaya ya shule mankubaliana kutumia mchakato wa upatanishi lakini bado hamjafikia makubaliano, mwishoni mwa kipindi cha suluhisho cha siku 30 za kalenda mchakato wa upatanishi unaweza kuendelea hadi makubaliano yafikiwe ikiwa wahusika wote wawili wanakubali uendeleaji kwa njia ya maandishi. Hata hivyo, ikiwa wewe au wilaya ya shule itajiondoa kwenye mchakato wa upatanishi wakati wa kipindi cha uendeleaji huu, basi muda wa siku 45 za kalenda kwa ajili ya kesi ya mchakato wa haki utaanza siku inayofuata.

**Makubaliano ya suluhu kwa njia ya maandishi**
Ikiwa suluhisho la mgogoro limefikiwa kwenye mkutano wa suluhisho, wewe na wilaya ya shule lazima muwe kwenye makubaliano yanayobana kisheria ambayo:

(1) Yanatiwa sahihi na wewe na mwakilishi wa wilaya ya shule aliye na mamlaka ya kubana wilaya ya shule; na
(2) Yanatekelezeka katika mahakama yoyote ya Jimbo yenye uwezo (mahakama ya Jimbo yenye mamlaka ya kusikia aina hii ya kesi) au katika mahakama ya wilaya ya Marekani au na Shirika la Elimu ya Jimbo, ikiwa Jimbo lako lina mbinu au taratibu nyingine zinazowaruhusu wahusika kujaribu utekelezaji wa makubaliano ya suluhisho.

**Kipindi cha ukaguzi wa makubaliano**
Ikiwa wewe na wilaya mtakuwa kwenye makubaliano kutokana na mkutano wa suluhisho, mhusika yeyote (wewe au wilaya ya shule) anaweza kuepuka makubaliano ndani ya siku 3 za kazi za muda ambao wewe na wilaya ya shule mlitia sahihi makubaliano.

## ***<u>KESI ZA MALALAMISHI YA MCHAKATO WA HAKI</u>***

***KESI YA MCHAKATO WA HAKI USIOPENDELEA***
***34 CFR §300.511***
**Jumla**
Kila wakati malalamishi ya mchakato wa haki yanapowasilihwa, wewe au wilaya ya shule inayohusika katika mgogoro lazima ipate fursa ya kesi ya mchakato wa haki usiipendelea, kama ilivyoelezwa katika sehemu za ***Malalamishi ya Mchakato wa Haki*** na ***Mchakato wa Suluhisho***.

**Hakimu asiyependelea**
Kwa kiwango cha chini, hakimu:

1. Hapaswi kuwa mwajiriwa wa Shirika la Elimu ya Jimbo wala wilaya ya shule ambayo inahusika katika elimu au utunzaji wa mtoto. Hata hivyo, mtu si mwajiriwa wa shirika kwa sababu analipwa na shirika ili kuhudumia hakimu;
2. Hapaswi kuwa na maslahi ya binafsi au ya taaluma ambayo yanagongana na lengo la hakimu katika kesi;
3. Lazima awe na maarifa na uelewa wa vipengele vya kanuni za IDEA, Serikali Kuu na Jimbo kuhusu IDEA na fasiri za kisheria za IDEA na mahakama ya Serikali Kuu na Jimbo; **<u>na</u>**
4. Lazima awe na maarifa na uwezo wa kusimamia kesi na kufanya na kuandika maamuzi, kulingana na desturi za kisheria zinazofaa na wastani.

Lazima kila wilaya ya shule ihifadhi orodha ya watu wanaohudumu kama mahakimu inayojumuisha taarifa za kuhitimu kwa kila hakimu.

**Suala la kesi ya mchakato wa haki**
Mhusika (wewe au wilaya ya shule) anayeomba kesi ya uchunguzi wa haraka hapaswi kuibua masuala kwenye kesi ya mchakato wa haki, isipokuwa mhusika mwingine akubali.

**Muda wa kuomba usikilizaji kesi**
Wewe au wilaya ya shule lazima iombe usikilizaji kesi usiopendelea kuhusu malalamishi ya mchakato wa haki ndani ya miaka miwili ya tarehe ambayo wewe au wilaya ya shule ilijua au ilipaswa kujua kuhusu suala lililoshughulikiwa katika malalamishi.

**Vighairi vya muda**
Muda ulio hapo juu hautumiki kwako ikiwa hukuweza kuwasilisha malalamishi ya mchakato wa haki kwa sababu:
1. Wilaya ya shule ilipotosha kwamba ilikuwa imetatua tatizo au suala unaloibua katika malalamishi; au
2. Wilaya ya shule ilizuia taarifa kutoka kwako ambazo zilihitajika kukupa chini ya Sehemu ya B ya IDEA.

***HAKI ZA USIKILIZAJI KESI***
***34 CFR §300.512***
**Jumla**
Una haki ya kujiwakilisha kwenye kesi ya mchakato wa haki (ikiwemo kesi inaayohusiana na taratibu za nidhamu) au rufaa ya kupokea au kupata ushahidi wa wajumbe, kama ilivyoelezwa kwa kichwa kidogo ***Rufaa ya Maamuzi; ukaguzi usiopendelea***. Zaidi ya hayo, mhusika yeyote kwenye kesi ana haki ya:
1. Kuandamana na kushauriwa na wakili na/au watu walio na maarifa au mafunzo maalum kuhusu matatizo ya watoto walio na ulemavu;
2. Kuwakilishwa na wakili kwenye kesi;
3. Kuwasilisha ushahidi na kupinga, kuhoji na kuhitaji mashahidi kuhudhuria;
4. Kuzuia kuwasilisha ushahidi wowote kwenye kesi ambao haujafichuliwa kwa mhusika mwingine angalau siku tano za kazi kabla ya kesi;
5. Kupata rekodi ya kesi ya maandishi, au, kwa chaguo lako, elektroniki, neno kwa neno; **na**
6. Kupata maoni na maamuzi ya maandishi, au, kwa chaguo lako, elektroniki.

**Ufichuaji wa ziada wa taarifa**

Siku zisizopungua tano za kazi kabla ya kesi ya mchakato wa haki, wewe na wilaya ya shule lazima mfichuliane tathmini zote zilizokamilishwa kufikia tarehe hiyo na mapendekezo kulingana na tathmini hizo ambazo wewe au wilaya ya shule mnakusudia kutumia kwenye kesi.
Hakimu anaweza kumzuia mhusika yeyote anayeshindwa kutii matakwa haya kuwasilisha tathmini au pendekezo muhimu kwenye kesi bila idhini ya mhusika mwingine.

**Haki za mzazi kwenye kesi**
Lazima upewe haki ya:
1. Kuwa na mtoto wako kwenye kesi;
2. Kufungulia umma kesi; **na**
3. Kupewa rekodi ya kesi, maoni na maamuzi bila malipo kwako.

***MAAMUZI YA KESI***
***34 CFR §300.513***
**Uamuzi wa hakimu**
Uamuzi wa hakimu kuhusu ikiwa mtoto wako alipokea elimu ya umma inayofaa bila malipo (FAPE) lazima utokane na ushahidi na hoja zinazohusiana moja kwa moja na FAPE.
Katika masuala yanayodai ukiukaji wa taratibu (kama vile "Timu ya IEP isiyokamilika"), hakimu anaweza kuamua mtoto wako hakupokea FAPE ikiwa tu ukiukaji wa taratibu:
1. Ulihitilafiana na haki ya mtoto wako ya elimu ya umma inayofaa bila malipo (FAPE);
2. Ulihitilafiana sana na fursa yako ya kushiriki katika mchakato wa kufanya maamuzi kuhusu utoaji wa elimu ya umma inayofaa bila malipo (FAPE) kwa mtoto wako; **au**
3. Ulisababisha mtoto wako kunyimwa manufaa ya elimu.

Hamna kati ya vipengele vilivyoelezwa hapo juu vinaweza kufasiriwa kuzuia hakimu kuagiza wilaya ya shule kutii matakwa yaliyo katika sehemu ya taratibu za ulinzi ya kanuni za Serikali Kuu kulingana na Sehemu ya B ya IDEA (34 CFR §§300.500 kupitia 300.536).

**Ombi tofauti la kesi ya mchakato wa haki**
Hakuna kitu katika sehemu ya taratibu za ulinzi ya kanuni za Serikali Kuu kulingana na Sehemu ya B ya IDEA (34 CFR §§300.500 kupitia 300.536) kinaweza kufasiriwa kukuzuia kuwasilisha malalamishi tofauti ya mchakato wa haki kuhusu suala tofauti na malalamishi ya mchakato wa haki ambayo tayari yamewasilishwa.

**Maoni na uamuzi kupelekwa kwenye jopo la ushauri na umma kwa jumla**
Shirika la Elimu ya Jimbo au wilaya ya shule, (yoyote iliyowajibikia kesi yako) baada ya kufuta taarifa yoyote ya kutambulisha binafsi, lazima:

1. Itoe maoni na maamuzi katika kesi ya mchakato wa haki au rufaa kwa jopo la ushauri wa elimu maalum ya Jimbo; **na**
2. Iwezeshe maoni na maamuzi hayo kupatikana kwa umma.

## ***RUFAA***

***MWISHO WA UAMUZI; RUFAA; UKAGUZI USIOPENDELEA***
***34 CFR §300.514***
**Mwisho wa uamuzi wa kesi**
Uamuzi unaotolewa katika kesi ya mchakato wa haki (ikiwa ni pamoja na kesi inayohusiana na taratibu za nidhamu) ni wa mwisho, isipokuwa mhusika yeyote katika kesi (wewe au wilaya ya shule) akate rufaa ya uamuzi kwa kuwasilisha kesi ya kiraia, kama ilivyoelezwa chini ya kichwa ***Kesi za Kiraia, Ikiwa ni Pamoja na Kipindi cha Kuwasilisha Kesi Hizo***.

***MUDA NA UFAAFU WA KESI NA UKAGUZI***
***34 CFR §300.515***
Lazima Shirika la Elimu ya Jimbo lihakikishe kuwa hazipiti zaidi ya dakika 45 za kalenda baada ya mwisho wa kipindi cha siku 30 za kalenda kwa mikutano ya suluhisho au kama ilivyoelezwa chini ya kichwa ***Marekebisho kwenye kipindi cha suluhisho cha siku 30 za kalenda***, si zaidi ya siku 45 za kalenda baada ya mwisho wa kipindi kilichorekebishwa.

1. Uamuzi wa mwisho unafikiwa katika kesi; na
2. Nakala ya uamuzi inatumwa kwa kila mhusika. Hakimu anaweza kuruhusu nyongeza mahususi ya muda zaidi ya kipindi cha siku 45 za kalenda kilichoelezwa hapo juu kwa ombi la mhusika yeyote (wewe au wilaya ya shule). Lazima kila kesi ifanywe wakati na mahali ambapo panakufaa wewe na mtoto wako.

***KESI ZA KIRAIA, IKIWA NI PAMOJA NA KIPINDI CHA KUWASILISHA KESI HIZO***
***34 CFR §300.516***
**Jumla**
Mhusika yeyote (wewe au wilaya ya shule) asiyekubali maoni na uamuzi katika kesi ya mchakato wa haki (ikiwa ni pamoja na kesi inayohusiana na taratibu za nidhamu) ana haki ya kuwasilisha kesi ya kiraia kulingana na suala ambalo lilikuwa chanzo cha kesi ya mchakato wa haki. Kesi inaweza kuwasilishwa katika mahakama ya Jimbo yenye uwezo (mahakama ya Jimbo yaliyo na mamlaka ya kusikiliza aina hii ya kesi) au katika mahakama ya wilaya ya Marekani bila kujali kiasi cha fedha za mgogoro.

**Kikomo cha muda**
Mhusika (wewe au wilaya ya shule) anayeleta kesi atakuwa na siku 42 za kalenda kutoka tarehe ya uamuzi wa hakimu kuwasilisha kesi ya kiraia.
IDAPA 08.02.03.109.05g

**Taratibu za ziada**
Katika kesi yoyote ya kiraia, mahakama:

1. Hupokea rekodi za kesi za usimamizi;
2. Husikiliza ushahidi wa ziada kwa ombi lako au kwa ombi la wilaya ya shule; **na**
3. Hutoa uamuzi wake kulingana na uzito wa ushahidi na kutoa suluhu ambayo mahakama inaona inafaa.

Chini ya hali zinazofaa, suluhu ya mahakama inaweza kujumuisha ulipaji wa gharama ya karo ya shule ya binafsi na huduma za elimu ya kufidia.

**Mamlaka ya mahakama ya wilaya**
Mahakama ya wilaya ya Marekani yana mamlaka ya kuamua kuhusu kesi zilizowasilishwa chini ya Sehemu ya B ya IDEA bila kujali kiasi cha fedha za mgogoro.

**Sheria za makubaliano**

Hakuna chochote katika Sehemu ya B ya IDEA kinachozuia au kuwekea kikomo haki, taratibu na suluhu zilizopo chini ya Katiba ya Marekani, Sheria ya Wamarekani Walio na Ulemavu ya 1990, Title V ya Sheria ya Urekebishaji ya 1973 (Kifungu cha 504), au sheria nyingine za Serikali Kuu zinazolinda haki za watoto walio na ulemavu, isipokuwa kabla ya kuwasilisha kesi ya kiraia kulingana na sheria hizi ukitafuta fidia ambayo pia inapatikana Sehemu ya B ya IDEA, taratibu za mchakato wa haki zilizoelezwa hapo juu lazima zitumike kwa kiwango sawa na kinachohitajika ikiwa mhusika amewasilisha kesi chini ya Sehemu ya B ya IDEA. Hii inamaanisha kwamba huenda ukapata suluhu chini ya sheria nyingine zinazopishana na zile zilizopo chini ya IDEA, lakini kwa jumla, kupata suluhu chini ya sheria hizo nyingine, lazima kwanza utumie suluhu za usimamizi zilizopo chini ya IDEA (yaani, malalamishi ya mchakato wa haki; mchakato wa suluhisho, ikiwa ni pamoja na mkutano wa suluhisho; na taratibu za kesi ya mchakato wa haki bila upendeleo) kabla ya kuenda mahakamani moja kwa moja.

***MAZINGIRA YA ELIMU YA MTOTO WAKATI MALALAMISHI YA MCHAKATO WA HAKI NA KESI ZINAPOSUBIRI***
***34 CFR §300.518***

Isipokuwa kama ilivyobainishwa hapa chini ya kichwa ***TARATIBU WAKATI WA KUWAADHIBU WATOTO WALIO NA ULEMAVU***, pindi malalamishi ya mchakato wa haki yanapotumwa kwa mhusika mwingine, wakati wa mchakato wa suluhisho na unaposubiri uamuzi wa kesi yoyote ya mchakato wa haki bila upendeleo au kesi ya mahakama, isipokuwa wewe na Jimbo au wilaya ya shule mkubaliane vinginevyo, lazima mtoto wako asalie katika mazingira yake ya sasa ya elimu.

Ikiwa malalamishi ya mchakato wa haki yanahusisha ombi la usajili wa mwanzo kwenye shule ya umma, lazima mtoto wako awekwe katika mpango wa shule ya umma wa mara kwa mara kwa idhini yako hadi ukamilishaji wa hatua hizo zote za kisheria.

Ikiwa malalamishi ya mchakato wa haki yanahusisha ombi la huduma za mwanzo chini ya Sehemu ya B ya IDEA kwa mtoto ambaye anapiga hatua kutoka kutumikiwa chini ya Sehemu ya C ya IDEA hadi Sehemu ya B ya IDEA na ambaye hastahiki tena huduma za Sehemu ya C kwa sababu mtoto amefikisha umri wa miaka mitatu, wilaya ya shule haihitajiki kutoa huduma za Sehemu ya C ambazo mtoto amekuwa akipokea. Mtoto akisemekana kustahiki chini ya Sehemu ya B ya IDEA na umwidhinishe kupokea elimu maalum na huduma husika kwa mara ya kwanza, ukisubiri matokeo ya hatua za kisheria, lazima wilaya ya shule itoe elimu maalum na huduma hizo husika ambazo hazipingwi (zile ambazo wewe na wilaya ya shule mnakubaliana).

Ikiwa hakimu katika kesi ya mchakato wa haki inayoendeshwa na Shirika la Elimu ya Jimbo atakubaliana nawe kwamba ubadilishaji wa mazingira ya elimu ya mtoto unafaa, lazima mazingira hayo yachukuliwe kama mazingira ya sasa ya elimu ya mtoto wako ambapo mtoto wako atasalia huku ukisubiri uamuzi wa kesi ya mchakato wa haki bila upendeleo au hatua yoyote ya kisheria ya mahakama.

***ADA YA WAKILI***
***34 CFR §300.517***
**Jumla**
Katika kesi au hatua yoyote ya kisheria inayoletwa chini ya Sehemu ya B ya IDEA, mahakama, kwa busara yake, yanaweza kukupa ada ya wakili inayofaa kama sehemu ya gharama, ukishinda.
Katika kesi au hatua yoyote ya kisheria inayoletwa chini ya Sehemu ya B ya IDEA, mahakama, kwa busara yake, yanaweza kulipatia Shirika la Elimu ya Jimbo au wilaya ya shule inayoshinda, ada ya wakili inayofaa kama sehemu ya gharama itakayolipwa na wakili, ikiwa wakili: (a) amewasilisha malalamishi au kesi ya mahakama ambayo mahakama yanaamua haina uzito, haifai, au haina msingi; **au** (b) ameendelea kuwasilisha madai baada ya madai kubainika kuwa yasiyo na uzito, yasiyofaa, au yasiyo na msingi; **au**
Katika kesi au hatua yoyote ya kisheria inayoletwa chini ya Sehemu ya B ya IDEA, mahakama, kwa busara yake, yanaweza kulipatia Shirika la Elimu ya Jimbo au wilaya ya shule inayoshinda, ada ya wakili inayofaa kama sehemu ya gharama itakayolipwa na wewe au wakili wako, ikiwa ombi lako la kesi ya mchakato wa haki au kesi ya mahakama ya baadaye iliwasilishwa kwa madhumuni yoyote yasiyofaa, kama vile kusumbua, kusababisha ucheleweshaji usiohitajika au kuongeza gharama isiyohitajika ya kesi au hatua ya kisheria (kesi).

**Uamuzi wa ada**
Mahakama yanaamua ada za wakili zinazofaa kama ifuatavyo:

1. Lazima ada zitegemee viwango vilivyo katika jamii ambayo kesi au hatua ya kisheria imetoka kwa ajili ya aina na ubora ya huduma zilizotolewa. Hakuna bonasi wala kizidishaji kitakachotumiwa kukokotoa ada zilizoamuliwa.
2. Ada ya wakili haitaamuliwa na gharama husika hazitalipwa katika kesi au hatua yoyote ya kisheria chini ya Sehemu ya B ya IDEA kwa huduma zilizotolewa baada ya kupewa ahadi ya malipo ya maandishi ikiwa:
   (a) Ahadi inatolewa ndani ya muda ulioelezwa na Sheria ya 68 ya Sheria za Taratibu za Kanuni au, wakati wa kesi ya mchakato wa haki au ukaguzi wa ngazi ya Jimbo, wakati wowote zaidi ya siku 10 za kalenda kabla ya hatua ya kisheria kuanza;
   (b) Ahadi haikubaliwi ndani ya siku 10 za kalenda; **na**
   (c) Mahakama au hakimu ya usimakizi anaamua kwamba suluhu uliyochukua haikufai kuliko ahadi ya pesa
   
   Licha ya vikwazo hivi, uamuzi wa ada ya wakili na gharama husika unaweza kupewa wewe ukishinda na kuwa na sababu ya kuridhisha kukataa ahadi ya pesa. Huenda ada isiamuliwe kuhusiana na mkutano wowote wa Timu ya mpango wa elimu iliyobinafsishwa (IEP) isipokuwa mkutano ufanywe kutokana na kesi ya usimamizi au kesi ya mahakama.
3. Pia huenda ada isiamuliwe kwa upatanishi kama ilivyoelezwa chini ya kichwa ***Upatanishi***.
   Mkutano wa suluhisho, kama ilivyoelezwa chini ya kichwa ***Mchakato wa Suluhisho***, unachukuliwa kuwa mkutano uliofanywa kutokana na kesi ya usimamizi au kesi ya mahakama na pia hauchukuliwi kuwa kesi ya usimamizi wala kesi ya mahakama kwa madhumuni ya vipengele hivi vya ada ya wakili.

Mahakama yanapunguza, inavyofaa, kiasi cha ada ya wakili iliyoamuliwa chini ya Sehemu ya B ya IDEA, ikiwa mahakama yanaamua kwamba:

1. Wewe, au wakili wako, wakati wa kesi au hatua ya kisheria, alichelewesha suluhisho la mwisho la mgogoro bila sababu;
2. Kiasi cha ada ya wakili kilichoidhinishwa kutolewa kinazidi kiwango cha kila saa kinachotozwa katika jamii kwa huduma sawa na mawakili wa ujuzi, sifa na tajriba sawa;
3. Muda uliotumika na huduma zilizotolewa zilikuwa zaidi kwa kuzingatia hali ya kesi au hatua ya kisheria; **au**
4. Wakili anayekuwakilisha hakuipa wilaya ya shule taarifa zinazofaa zilizo katika notisi ya ombi la mchakato wa haki kama ilivyoelezwa chini ya kichwa ***Malalamishi ya Mchakato wa Haki.***

Hata hivyo, mahakama hayatapunguza ada ikiwa yataamua kuwa Jimbo au wilaya ya shule ilichelewesha bila sababu suluhisho la mwisho la kesi au hatua ya kisheria au kulikuwa na ukiukaji chini ya vipengele vya taratibu za ulinzi vya Sehemu ya B ya IDEA.

## ***<u>TARATIBU WAKATI WA KUWAADHIBU WATOTO WALIO NA ULEMAVU</u>***

***MAMLAKA YA WATUMISHI WA SHULE***
***34 CFR §300.530***

**Uamuzi kulingana na hali**

Watumishi wa shule wanaweza kufikiria jambo lolote la kipekee kulingana na kila hali wakati wa kuamua ikiwa ubadilishaji wa mazingira ya elimu, ulifanywa kwa mujibu wa matakwa yafuatayo ambayo yanahusiana na nidhamu, unamfaa mtoto aliye na ulemavu ambaye anakiuka kanuni ya shule ya maadili ya wanafunzi.

**Jumla**

Kwa kiwango ambacho pia wanachukua hatua hiyo kwa watoto wasio na ulemavu, watumishi wa shule wanaweza, kwa **siku zisizozidi 10 za shule** mfululizo, kumwondoa mtoto aliye na ulemavu ambaye anakiuka maadili ya wanafunzi kwenye mazingira yake ya elimu ya sasa hadi kwenye mazingira mbadala ya elimu ya muda mfupi, mazingira mengine ya elimu au kuondoshwa shuleni kwa muda mfupi. Watumishi wa shule pia wanaweza kuweka hatua za kuondoa za ziada za mtoto zisizozidi **siku 10 za shule** mfululizo katika mwaka uleule wa shule kwa matukio tofauti ya mwenendo mbaya, mradi tu hatua hizo za kuondoa hazitajumuisha ubadilishaji wa mazingira ya elimu (angalia kichwa ***Ubadilishaji wa Mazingira ya Elimu Kwa Sababu ya Hatua za Kuondoa za Nidhamu*** za ufafanuzi).

Pindi tu mtoto aliye na ulemavu anapoondolewa kwenye mazingira yake ya sasa ya elimu kwa jumla ya siku 10 za shule katika mwaka uleule wa shule, lazima wilaya ya shule, wakati wa siku zozote zinazofuata za kuondolewa katika mwaka huo wa shule, itoe huduma kwa kiwango kinachohitajika hapa chini ya kichwa Huduma.

**Mamlaka ya ziada**

Ikiwa tabia iliyokiuka kanuni ya maadili ya wanafunzi haikuwa uhusiano wa ulemavu wa mtoto (angalia kichwa ***Uamuzi wa uhusiano***) na mabadiliko ya nidhamu ya mazingira ya elimu yazidi siku 10 za shule mfululizo, watumishi wa shule wanaweza kutumia taratibu za nidhamu kwa mtoto huyo aliye na ulemavu kwa njia sawa na kwa muda sawa kama ambavyo wangefanya kwa watoto wasio na ulemavu, isipokuwa lazima shule impe mtoto huduma kama ilivyoelezwa hapa chini ya ***Huduma***. Timu ya ya mtoto ya IEP inaamua mazingira ya muda mfupi ya elimu mbadala kwa huduma hizo.

**Huduma**

Wilaya ya shule haimpi huduma mtoto aliye na ulemavu au asiye na ulemavu ambaye ameondolewa kwenye mazingira yake ya elimu ya sasa kwa ***siku 10 za shule au chache*** katika mwaka huo wa shule.

Mtoto aliye na ulemavu ambaye ameondolewa kwenye mazingira ya elimu ya sasa ya mtoto kwa ***zaidi ya siku 10 za shule*** na tabia si uhusiano wa ulemavu wa mtoto (angalia kichwa, Uamuzi wa uhusiano) au ambaye ameondolewa chini ya hali za kipekee (angalia kichwa, Hali maalum) lazima:

1. Aendelee kupokea huduma za elimu (apate elimu ya umma inayofaa bila malipo), ili kumwezesha mtoto kuendelea kushiriki katika mtaala wa elimu ya jumla, ingawa katika mazingira mengine ya elimu (ambayo yanaweza kuwa mazingira ya muda mfupi ya elimu mbadala) na kupiga hatua ya kutimiza malengo yaliyowekwa katika IEP ya mtoto; **<u>na</u>**
2. Afanye, inavyofaa, tathmini ya tabia ya utendaji na huduma za mikakati tabia na mabadiliko, ambavyo vimeundwa ili kuangazia ukiukaji wa tabia ili isirudiwe tena.

Baada ya mtoto aliye na ulemavu kuondolewa kwenye mazingira yake ya elimu kwa **siku 10 za shule** katika mwaka huohuo wa shule na **<u>ikiwa</u>** kuondolewa ni kwa **siku 10 za shule** mfululizo au chini **<u>na</u>** ikiwa kuondolewa si mabadiliko ya mazingira ya elimu (angalia ufafanuzi hapa chini), **<u>basi</u>** watumishi wa shule, kwa ushirikiano na angalau mmoja wa walimu wa mtoto, wanaamua kiwango ambacho huduma zinahitajika ili kumwezesha mtoto kuendelea kushiriki katika mtaala wa elimu ya jumla, ingawa katika mazingira mengine ya elimu na kuendelea kutimiza malengo yaliyobainishwa katika IEP ya mtoto.

Ikiwa kuondolewa ni mabadiliko ya mazingira ya elimu (angalia kichwa, ***Mabadiliko ya Mazingira ya Elimu*** Kwa Sababu ya Kuondolewa Kutokana na Nidhamu), Timu ya IEP ya mtoto inaamua huduma zinazofaa ili kumwezesha mtoto kuendelea kushiriki katika mtaala wa elimu ya jumla, ingawa katika mazingira mengine ya elimu (yanayoweza kuwa mazingira ya muda mfupi ya elimu mbadala) na kuendelea kutimiza malengo yaliyobainishwa katika IEP ya mtoto.

**Uamuzi wa uhusiano**

Ndani ya **siku 10 za shule** za uamuzi wowote wa kubadilisha mazingira ya elimu ya mtoto aliye na ulemavu kwa sababu ya

ukiukaji wa kanuni ya maadili ya mwanafunzi (isipokuwa kwa kuondolewa ambako ni kwa **siku 10 za shule** mfululizo au chache na si mabadiliko ya mazingira ya elimu), wilaya ya shule, wewe na washirika wengine wa Timu ya IEP (kama ilivyoamuliwa nawe na wilaya ya shule) lazima mkague taarifa zote muhimu zilizo katika faili ya mtoto, ikiwa ni pamoja na IEP ya mtoto, maoni yoyote ya mwalimu na taarifa yoyote muhimu ulizotoa ili kuamua:

1. Ikiwa maadili yanayozungumziwa yalisababishwa na, au yalikuwa na uhusiano wa moja kwa moja na mkubwa kwenye ulemavu wa mtoto; **au**
2. Ikiwa maadili yanayozungumziwa yalikuwa matokeo ya moja kwa moja ya kosa la wilaya ya shule kutekeleza IEP ya mtoto.

Ikiwa wilaya ya shule, wewe na washirika wengine muhimu wa Timu ya IEP ya mtoto mnaamua kwamba masharti hayo yote yalitimizwa, lazima maadili yaamuliwe kuwa uhusiano wa ulemavu wa mtoto.

Ikiwa wilaya ya shule, wewe, na washirika wengine muhimu wa Timu ya IEP ya mtoto mtaamua kwamba maadili yanayozungumziwa yalikuwa matokeo ya moja kwa moja ya kosa la wilaya ya shule kutekeleza IEP, lazima wilaya ya shule ichukue hatua ya haraka kusuluhisha kasoro hizo.

**Uamuzi kwamba tabia ilikuwa uhusiano wa ulemavu wa mtoto**

Ikiwa wilaya ya shule, wewe na washirika wengine muhimu wa Timu ya IEP mtaamua kwamba mwenendo ulikuwa uhusiano wa ulemavu wa mtoto, lazima Timu ya IEP:

1. Ifanye tathmini ya tabia ya utendaji, isipokuwa wilaya ya shule iwe ilifanya tathmini ya tabia ya utendaji kabla ya tabia iliyosababisha mabadiliko ya mazingira ya elimu kutokea na kutekeleza mpango wa mwingilio wa tabia wa mtoto; **au**
2. Ikiwa mpango wa mwingilio wa tabia tayari umeundwa, ikague mpango wa mwingilio wa tabia na kuurekebisha, inavyohitajika, kuangazia tabia.

Isipokuwa kama ilivyoelezwa hapa chini ya kichwa ***Hali za kipekee***, lazima wilaya ya shule imrejeshe mtoto wako kwenye mazingira ya elimu ambayo mtoto wako aliondolewa, isipokuwa wewe na wilaya mkubali kubadilisha mazingira kama sehemu ya marekebisho ya mpango wa mwingilio wa tabia.

**Hali za kipekee**

Iwe tabia ilikuwa au haikuwa ya uhusiano wa ulemavu wa mtoto wako, watumishi wa shule wanaweza kumwondoa mwanafunzi hadi kwenye mazingira ya muda mfupi ya elimu mbadala (yanayoamuliwa na Timu ya IEP ya mtoto) kwa muda usiozidi siku 45 za shule, ikiwa mtoto wako:

1. Anabeba silaha (angalia ufafanuzi hapa chini) shuleni au ana silaha shuleni, kwenye jengo la shule, au kwenye hafla ya shule chini ya mamlaka ya Shirika la Elimu ya Jimbo au wilaya ya shule;
2. Ana au hutumia dawa haramu kwa kujua (angalia ufafanuzi hapa chini), au anauza au anashawishi uuzaji wa mihadarati inayodhibitiwa, (angalia ufafanuzi hapa chini), akiwa shuleni, kwenye jengo la shule, au kwenye hafla ya shule chini ya mamlaka ya Shirika la Elimu ya Jimbo au wilaya ya shule; **au**
3. Amesababisha majeraha mabaya ya kimwili (angalia ufafanuzi hapa chini) kwa mtu mwingine shuleni, kwenye jengo la shule, au kwenye hafla ya shule chini ya mamlaka ya Shirika la Elimu ya Jimbo au wilaya ya shule.

**Fafanuzi**
***Mihadaharati inayodhibitiwa*** inamaanisha dawa za kulevya au mihadarati mingine inayotambuliwa chini ya viambatisho I, II, III, IV, au V katika kifungu 202(c) cha Sheria ya Mihadarati Inayodhibitiwa (21 U.S.C. 812(c)).
***Dawa haramu*** inamaanisha mihadarati inayodhibitiwa; lakini haijumuishi mihadarati inayodhibitiwa ambayo inayomilikiwa kisheria au inayotumiwa chini ya usimamizi wa mtaalamu wa huduma ya afya aliye na leseni au ambayo inamilikiwa kisheria au kutumiwa chini ya mamlaka mengine yoyote chini ya Sheria hiyo au chini ya kipengele kingine chochote cha Sheria ya Serikali Kuu.
***Majeraha mabaya ya kimwili*** maana yake imepewa msamiati ''majeraha mabaya ya kimwili'' chini ya aya ya (3) ya kijifungu (h) cha kifungu 1365 cha anwani 18, Kanuni ya Marekani.
***Silaha*** maana yake imepewa msamiati ''silaha hatari'' chini ya aya ya (2) ya kijifungu cha kwanza (g) cha kifungu 930 cha anwani 18, Kanuni ya Marekani.

**Arifa**
Tarehe ambayo inafanya uamuzi wa kuondoa ambako ni kubadilisha mazingira ya elimu ya mtoto wako kwa sababu ya ukiukaji wa kanuni ya maadili ya mwanafunzi, lazima wilaya ya shule ikuarifu kuhusu uamuzi huo na kukupa notisi ya taratibu za ulinzi.

***MABADILIKO YA MAZINGIRA YA ELIMU KWA SABABU YA KUONDOLEWA KWA NIDHAMU***
***34 CFR §300.536***
Kuondolewa kwa mtoto wako aliye na ulemavu kwenye mazingira ya sasa ya elimu ya mtoto wako ni mabadiliko ya mazingira ya elimu ikiwa:

1. Kuondolewa ni kwa zaidi ya siku 10 za shule mfululizo; **<u>au</u>**
2. Mtoto wako ameondolewa mara kadhaa hali inayosababisha mtindo kwa sababu:
   (a) Mara za kuondolewa ni jumla ya zaidi ya siku 10 za shule katika mwaka wa shule;
   (b) Tabia ya mtoto wako ni sawa na tabia ya mtoto katika matukio ya awali yaliyosababisha kuondolewa mara kadhaa; na
   (c) Mambo kama hayo ya ziada kama urefu wa kila hatua ya kuondolewa, jumla ya kiwango cha muda ambao mtoto wako ameondolewa na ukaribu wa hatua za kuondolewa.

Iwe mtindo wa kuondolewa unahusisha mabadiliko ya mazingira ya elimu unaamuliwa kulingana na hali na wilaya ya shule na, ukipingwa, utakaguliwa kupitia mchakato wa haki na hatua za kisheria.

***KUAMUA MAZINGIRA YA ELIMU***
***34 CFR §300.531***
Timu ya mpango wa elimu iliyobinafsishwa (IEP) inaamua mazingira ya muda mfupi ya elimu mbadala kwa kuondolewa ambako ni **mabadiliko ya mazingira ya elimu**, na kuondolewa chini ya vichwa ***Mamlaka ya ziada*** na ***Hali za kipekee***.

***RUFAA34 CFR §300.532***
**Jumla**
Unaweza kuwasilisha malalamishi ya mchakato wa haki (angalia kichwa ***Taratibu za Malalamishi ya Mchakato wa Haki***) ili kuomba usikilizaji wa kesi ya mchakato wa haki ikiwa unapinga:

1. Uamuzi wowote kuhusu mabadiliko ya mazingira ya elimu yaliyofanywa chini ya vipengele hivi vya nidhamu; **<u>au</u>**
2. Uamuzi wa uhusiano ulioelezwa hapo juu.

Wilaya ya shule inaweza kuwasilisha malalamishi ya mchakato wa haki (angalia hapo juu) ili kuomba usikilizaji kesi ya mchakato wa haki ikiwa inaamini kwamba kudumisha mazingira ya elimu ya sasa ya mtoto wako kuna uwezekano mkubwa wa kusababisha majeraha kwa mtoto wako au wengine.

**Mamlaka ya hakimu**
Hakimu anayekidhi matakwa yaliyoelezwa chini ya kichwa ***Ofisa wa kesi asiyependelea*** lazima aendeshe usikilizaji wa kesi na kufanya uamuzi. Hakimu anaweza:
1. Kumrejesha mtoto wako aliye na ulemavu katika mazingira ya elimu ambayo mtoto wako aliondolewa ikiwa hakimu ataamua kwamba kuondolewa kulikuwa ukiukaji wa matakwa yaliyoelezwa chini ya kichwa ***Mamlaka ya Watumishi wa Shule***, au kwamba tabia ya mtoto wako ulikuwa uhusiano wa ulemavu wa mtoto wako; **au**
2. Kuagiza mabadiliko ya mazingira ya elimu ya mtoto wako aliye na ulemavu hadi kwenye mazingira ya muda mfupi ya elimu mbadala inayofaa kwa siku zisizozidi 45 za shule ikiwa hakimu ataamua kwamba kudumisha mazingira ya sasa ya mtoto wako kuna uwezekano mkubwa wa kusababisha majeraha kwa mtoto wako au wengine.

Taratibu hizi za kesi zinaweza kurudiwa, ikiwa wilaya ya shule inaamini kwamba kumrejesha mtoto wako kwenye mazingira asili ya elimu kuna uwezekano mkubwa wa kusababisha majeraha kwa mtoto wako au wengine.
Kila wakati wewe au wilaya ya shule inapowasilisha malalamishi ya mchakato wa haki ili kuomba usikilizaji kesi, lazima usikilizaji kesi ufanywe unaokidhi matakwa yaliyoelezwa chini ya vichwa ***Taratibu za Malalamishi ya Mchakato wa Haki, Kesi kuhusu Malalamishi ya Mchakato wa Haki***, isipokuwa kama ifuatavyo:
1. Lazima Shirika la Elimu ya Jimbo au wilaya ya shule iweke mpango wa kesi ya mchakato wa haki wa haraka, ambao lazima utokee ndani ya siku **20** za shule za tarehe ambayo usikilizaji kesi umeombwa na lazima usababishe kutokea kwa uamuzi ndani ya siku **10** za shule baada ya kesi.
2. Isipokuwa wewe na wilaya ya shule mkubaliane kwa njia ya maandishi kuondoa mkutano, au mkubali kutumia upatanishi, lazima mkutano wa suluhisho uwepo ndani ya siku **saba** za kalenda za kupokea notisi ya malalamishi ya mchakato wa haki. Kesi inaweza kuendelea isipokuwa suala liwe limesuluhishwa kwa kiwango kinachoridhisha wahusika wote wawili ndani ya siku **15** za kalenda za kupokea malalamishi ya mchakato wa haki.
3. Jimbo linaweza kuweka sheria za taratibu tofauti za kesi za mchakato wa haki za haraka kuliko lilizoweka kwa kesi nyingine za mchakato wa haki, lakini isipokuwa kwa muda, lazima sheria hizo zilingane na sheria zilizo katika waraka huu kuhusu kesi za mchakato wa haki.

Wewe au wilaya ya shule inaweza kukata rufaa ya uamuzi katika kesi ya mchakato wa haki iliyoharakishwa sawa na maamuzi katika kesi nyingine za mchakato wa haki (angalia kichwa ***Rufaa***).

***MAZINGIRA YA ELIMU WAKATI WA RUFAA***
***34 CFR §300.533***
Wakati, kama ilivyoelezwa hapo juu, wewe au wilaya ya shule ikiwasilisha malalamishi ya mchakato wa haki unaohusiana na masuala ya nidhamu, lazima mtoto wako (isipokuwa wewe na Shirika la Elimu ya Jimbo au wilaya ya shule mkubaliane vinginevyo) asalie katika mazingira ya muda mfupi ya elimu mbadala akisubiri uamuzi wa hakimu, au hadi mwisho wa kipindi cha kuondolewa kama ilivyobainishwa na kuelezwa chini ya kichwa Mamlaka ya Watumishi wa Shule, yoyote inayotangulia.

***ULINZI WA WATOTO AMBAO BADO HAWASTAHIKI ELIMU MAALUM NA HUDUMA HUSIKA***
***34 CFR §300.534***
**Jumla**
Ikiwa mtoto wako hajaamuliwa kustahiki elimu maalum na huduma husika na akiuke kanuni ya maadili ya wanafunzi, lakini wilaya ya shule ilifahamu (kama ilivyoamuliwa hapa chini) kabla ya tabia iliyosababisha hatua ya nidhamu kuchukuliwa kutokea, kwamba mtoto wako alikuwa mtoto aliye na ulemavu, basi mtoto wako anaweza kudai ulinzi wowote kati ya ule ulioelezwa katika notisi hii.

**Msingi wa ufahamu wa masuala ya nidhamu**
Wilaya ya shule itasemekana kufahamu kwamba mtoto wako ni mtoto aliye na ulemavu ikiwa, kabla ya tabia iliyosababisha hatua ya nidhamu kuchukuliwa kutokea:
1. Ulionyesha wasiwasi kwa njia ya maandishi kwa watumishi wa usimamizi kuhusu shirika la elimu linalofaa, au kwa mwalimu wa mtoto wako kwamba mtoto wako anahitaji elimu maalum na huduma husika;
2. Uliomba tathmini inayohusiana na ustahiki wa elimu maalum na huduma husika chini ya Sehemu ya B ya IDEA; **au**
3. Mwalimu wa mtoto wako au watumishi wengine wa wilaya ya shule walionyesha wasiwasi mahususi kuhusu mtindo wa tabia ambayo mtoto wako alionyesha moja kwa moja kwa mkurugenzi wa wilaya ya shule kuhusu elimu maalum au kwa

watumishi wengine wa usimamizi wa wilaya ya shule.

**Kighairi**

Wilaya ya shule haitasemekana kuwa na ufahamu huo ikiwa:

1. Hujaruhusu tathmini ya mtoto wako au umekataa huduma za elimu maalum; **au**
2. Mtoto wako ametathminiwa na kuamuliwa kutokuwa mtoto aliye na ulemavu chini ya Sehemu ya B ya IDEA.

**Masharti yanayotumika ikiwa hakuna msingi wa ufahamu**

Ikiwa kabla ya kuchukua hatua za nidhamu dhidi ya mtoto wako, wilaya ya shule haina ufahamu kwamba mtoto wako ni mtoto aliye na ulemavu, kama ilivyoelezwa hapo juu chini ya vichwa ***Msingi wa ufahamu wa masuala ya nidhamu*** na ***Kighairi***, huenda mtoto wako akachukuliwa hatua za nidhamu zinazotumika kwa watoto wasio na ulemavu ambao wanashiriki katika tabia zinazolingana.

Hata hivyo, ikiwa ombi litatolewa la tathmini ya mtoto wako wakati ambapo mtoto wako anachukuliwa hatua za nidhamu, lazima tathmini ifanywe kwa njia ya haraka.

Ikiwa tathmini haijakamilika, mtoto wako atasalia katika mazingira ya elimu yaliyoamuliwa na mamlaka ya shule, ambayo inaweza kujumuisha usimamishaji au kufukuzwa bila huduma za elimu.

Ikiwa mtoto wako ataamuliwa kuwa mtoto aliye na ulemavu, kwa kuzingatia taarifa kutoka kwenye tathmini iliyofanywa na wilaya ya shule na taarifa ulizotoa, lazima wilaya ya shule itoe elimu maalum na huduma husika kwa mujibu wa Sehemu ya B ya IDEA, ikiwa ni pamoja na matakwa ya nidhamu yaliyoelezwa hapo juu.

***RUFAA KWA NA HATUA INAYOCHUKULIWA NA MAMLAKA YA UTEKELEZAJI SHERIA NA MAMLAKA MAHAKAMA***
***34 CFR §300.535***

Sehemu ya B ya IDEA:

1. Haizuii shirika kuripoti uhalifu uliotekelezwa na mtoto aliye na ulemavu kwa mamlaka yanayofaa; **au**
2. Haizuii mamlaka ya Jimbo ya utekelezaji sheria na mamlaka ya mahakama kutekeleza majukumu kuhusiana na utumiaji wa sheria ya Serikali Kuu na Jimbo kwa uhalifu uliotekelezwa na mtoto aliye na ulemavu.

**Utoaji wa rekodi**

Wilaya ya shule ikiripoti uhalifu uliotekelezwa na mtoto aliye na ulemavu, wilaya ya shule:

1. Lazima ihakikishe kwamba nakala za elimu maalum ya mtoto na rekodi za nidhamu zinatolewa ili kuzingatiwa na mamlaka ambayo shirika linaripoti uhalifu kwayo; **na**
2. Inaweza kutoa nakala za elimu maalum na rekodi za nidhamu ya mtoto tu kwa kiwango kinachoruhusiwa na Sheria ya Haki na Faragha ya Elimu ya Familia (FERPA)

## ***MATAKWA YA MAZINGIRA YA ELIMU PAMOJA NA WAZAZI WA WATOTO WALIO KATIKA SHULE ZA BINAFSI KWA GHARAMA YA UMMA***

***JUMLA***
***34 CFR §300.148***
Sehemu ya B ya IDEA haihitaji wilaya ya shule ilipie gharama ya elimu, ikiwa ni pamoja na elimu maalum na huduma husika, za mtoto wako aliye na ulemavu kwenye shule au kituo cha binafsi ikiwa wilaya ya shule imewezesha kuwepo kwa elimu ya umma inayofaa bila malipo (FAPE) kwa mtoto wako na uchague kumweka mtoto wako katika shule au kituo cha binafsi. Hata hivyo, wilaya ya shule pale ambapo shule ya binafsi ipo lazima ijumuishe mtoto wako miongoni mwa watu ambao mahitaji yao yanashughulikiwa chini ya vipengele vya Sehemu ya B kuhusu watoto ambao wamawekwa na wazazi wao katika shule ya binafsi chini ya 34 CFR §§300.131 hadi 300.144.

**Malipo ya gharama ya mazingira ya shule ya binafsi**
Ikiwa mtoto wako alipokea elimu maalum na huduma husika awali chini ya mamlaka ya wilaya ya shule na ukachagua kumsajili mtoto wako katika shule ya chekechea, shule ya msingi au shule ya upili ya binafsi bila idhini ya au rufaa kutoka kwenye wilaya ya shule, mahakama au hakimu anaweza kuhitaji shirika kukulipa gharama ya usajili huo ikiwa mahakama au hakimu ataamua kwamba shirika halikuwa limewezesha uwepo wa elimu ya umma inayofaa bila malipo (FAPE) kwa mtoto wako wakati unaofaa kabla ya usajili huo na kuwa mazingira ya elimu ya binafsi yanafaa. Hakimu au mahakama yanaweza kuamua mazingira yako ya elimu yanafaa, hata ikiwa mazingira ya elimu hayakidhi viwango vya Jimbo vinavyotumika kwa elimu inayotolewa na Shirika la Elimu ya Jimbo na wilaya za shule.

**Vikomo kwenye malipo ya gharama**
Gharama ya malipo iliyoelezwa katika aya iliyo hapo juu inaweza kupunguzwa au kunyimwa:
1. Ikiwa: (a) Kwenye mkutano wa hivi majuzi wa mpango wa elimu iliyobinafsishwa (IEP) uliohudhuria kabla ya kumwondoa mtoto wako kwenye shule ya umma, hukufahamisha Timu ya IEP kwamba ulikuwa ukikataa mazingira ya elimu yaliyopendekezwa na wilaya ya shule kumpa mtoto wako FAPE, ikiwa ni pamoja na wasiwasi wako na kusudi lako la kumsajili mtoto wako katika shule ya binafsi kwa gharama ya umma; au (b) Siku zisizopungua 10 za kazi (ikiwa ni pamoja na sikukuu yoyote inayotokea siku ya kazi) kabla ya kuondolewa kwa mtoto wako kwenye shule ya umma, hukuipa wilaya ya shule notisi ya maandishi kuhusu taarifa hizo;
2. Ikiwa, kabla ya kumwondoa mtoto wako kwenye shule ya umma, wilaya ya shule ilikupa notisi ya maandishi mapema kuhusu kusudi lake la kutathmini mtoto wako (ikiwa ni pamoja na taarifa ya madhumuni ya tathmini iliyostahiki na iliyofaa), lakini hukumleta mtoto kwa ajili ya tathmini; **au**
3. Baada ya mahakama kuamua kwamba vitendo vyako havikufaa.

Hata hivyo, gharama ya malipo:
1. Haipaswi kupunguzwa wala kunyimwa kwa ajili kukosa kutoa notisi ikiwa: (a) Shule ilikuzuia kutoa notisi; (b) Hukuwa umepokea notisi ya jukumu lako la kutoa notisi iliyoelezwa hapo juu; au (c) Utii wa matakwa yaliyo hapo juu ungeweza kusababisha madhara ya kimwili kwa mtoto wako; na
2. Huenda, kwa busara ya mahakama au hakimu, isipunguzwe wala kunyimwa kwa kosa lako la kutotoa notisi inayohitajika ikiwa: (a) Huwezi kusoma wala kuandika kwa Kiingereza; au (b) Utii wa matakwa yaliyo hapo juu unaweza kusababisha madhara mabaya ya hisia kwa mtoto wako.